# *Yesu Kristo Yeye Yule Jana, Leo, Na Hata Milele*

. . . wewe sana, Ndugu.

2 Nilifurahi sana niliposikia wimbo huo, *Alishuka Kutoka Utukufuni Mwake*. Ndugu yeyote yule aliyeuimba huo, nilisikia aliuimba kwa heshima yangu, hakika ninathamini hilo, huo ndio wimbo ninaoupenda sana. Uliandikwa na rafiki msiri wangu, Ndugu William Booth-Clibborn.

3 Unaonyesha mle ndani Uungu wa Bwana wetu Yesu Kristo. Leo hii wanapojaribu kumfanya mtu mwingine tu, ama—ama nabii, ama chochote kile, nafikiri huo unaonyesha kile alichokuwa. Alishuka kutoka Utukufuni, Mungu alidhihirishwa katika mwili katika Kristo Yesu, Mwanawe, Ye—Ye—Yeye alionyesha katika mwili Wake kile Mungu alichokuwa. Naye Mungu anaweza kuonyesha kupitia kwetu kile alicho kama tu tutamruhusu. Kupitia haki ya Kristo, basi maovu yetu hayahesabiwi kwetu. Inahesabiwa, imani yetu inahesabiwa kwamba itahesabiwa kwetu kama imani na haki mbele Zake, ambayo, hatuna yetu wenyewe ambayo tungeweza kutoa.

4 Ninatumaini tu ya kwamba utakuwa ni wakati mzuri tena, ambapo ninaweza kurudi kwenye—kwenye mji huu. Asubuhi ya leo nilikuwa nikizungumza katika kusanyiko dogo linalopendeza sana hapa, kusanyiko linaloitikia sana. Najisikia kama tungeweza kukaa pamoja nanyi kwa muda kidogo tupate kufahamiana . . . Huduma yangu kidogo ni ya kipekee, na kwa hiyo haiwezekani kuielezea yote katika ibada moja ndogo, ndipo inawafanya kushangaa kuhusu *hili* ama *lile*. Lakini wakati tukizuru kwa muda mrefu, mwaweza kuona usiku baada ya usiku na kuangalia kile kilichonenwa na kuona kama kinatendeka, na ndipo mtaanza kutambua hii huduma ni nini, halafu inatufanya tuelewane vizuri zaidi.

5 Hakika ninathamini mwaliko ambao huyu mchungaji hapa alinipa kuja hapa kanisani, kwa ajili ya ninyi watu wote, na kwa ajili ya makanisa yote kote mjini. Natumaini siku moja, kama ni mapenzi ya Mungu, kwamba ningeweza kurudi na kukaa katika ibada ya muda mrefu zaidi humu mjini, ambapo tungeweza kuwaleta wa—watu wote pamoja, makanisa, wahudumu.

6 Na, usiku wa leo, inawatatiza sana wahudumu, labda wengi wa wagonjwa wao iliwabidi kupata kibali cha kushuka kuja kuombewa. Nami laiti ningaliweza kuelezea hisia zangu kwa wachungaji walioyaachilia makusanyiko yao usiku wa leo, wapate kuja kusikia ibada na kuombewa. Bwana na awabariki

daima watu kama hao, watu wenye—wenye ninii kubwa—wenye uadilifu mkubwa, mtu aliye na moyo halisi kwa ajili ya wagonjwa na wahitaji. Nina hakika ya kwamba watasitawi, katika kufanya mambo kama hayo.

7 Sasa, nafikiri kuna makanisa kadhaa hapa. Ndio kwanza nifungue barua dakika chache zilizopita kutoka kwa mchungaji wa First Assembly of God hapa mjini, naye alikuwa na mtu mgonjwa sana, hapa hospitalini. Na—na kama, sijui, yeye yuko kanisani wakati huu, nadhani, na hakika nitakuwa katika maombi kwa ajili ya mtu huyo, kama yeyote wa watu wao yuko hapa.

8 Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, kamwe hawezi kushindwa. Nami ninatumaini ya kwamba Yeye atambariki kila mmoja wetu usiku wa leo, nasi tutaondoka hapa tukiwa na utukufu wa Mungu moyoni mwetu.

9 Sasa, ningetaka kusema jambo hili, kwa sababu ya kupitia tu, na kuwaombea wagonjwa, na kusema ibada ya uponyaji, sasa, sisi, hiyo siyo huduma yangu yote, tunaamini jambo la kwanza ni wokovu, kwa sababu kama ukiponywa, ukiishi wakati wowote labda utakuwa mgonjwa tena, bali unapompokea Kristo, unao Uzima wa Milele. Na Uzima wa Milele ni zaidi sana vipi kuliko uponyaji wa mwili?

10 Lakini uponyaji wa Kiungu, Kristo aliutumia, uponyaji wa Kiungu, kuvutia usikivu wa watu. Na yapata asilimia themanini na sita ya huduma Yake ilikuwa katika uponyaji wa Kiungu. Kwa hiyo, ni kitu kinachoonyesha mambo ya kimbinguni.

11 Na sasa, yote ambayo yangeweza kufanywa kwa ajili ya mtu, kwa ajili yako, mimi, au mtu yeyote, yalikamilika na kumalizika pale Kalvari. Sasa, wakati mimi. . . wengi, nimewasikia wengi wakisema kwamba walikuwa na uponyaji mikononi mwao, na hiyo—hiyo huenda ikawa yote ni kweli, sijui, lakini jinsi ninavyoamini, ni kwamba uponyaji wetu umekamilika pamoja na wokovu wetu, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Ni wakati uliopita.

12 Sasa, njia pekee tunayoweza kupokea chochote kutoka kwa Mungu ni (Sasa shika hili.), si kutafuta kitu fulani, kusema, "Mkono wangu umelemaa, niliombewa, mkono wangu haunyooki katika dakika moja," hiyo haimaanishi sijaponywa. La, hilo halimaahishi hivyo, halina uhusiano wowote nalo, mnaona, kwa sababu nimeona katika miaka thelathini na mmoja katika huduma, miaka kumi na mitano kuzunguka na kuzunguka ulimwengu, kwamba wakati mwingine unapomwombea mtu, ingekuwa ni juma moja ama mawili kabla halijatukia.

13 Nami nilikuwa nikifikiria juu ya kisa fulani sasa hivi, mara nyingi nimekirejea, mama mmoja alikuja mkutanoni, na ilikuwa kwenye mstari wa maombi, ndipo Roho Mtakatifu akaanza

kumwambia kwamba yeye alikuwa ni nani na shida aliyokuwa nayo. Alikuwa na kidonda kibaya sana tumboni mwake, na—na ndipo akamwambia ya kwamba, hivyo ndivyo Roho Mtakatifu alivyokuwa akisema. Anajua ilibidi iwe ni kitu fulani kufunua hilo, akalitambua, naye alitaka kulitekeleza hilo.

14 Halafu chini mstarini mbele kidogo alikuwepo jirani yake, naye jirani yake alikuwa na kivimbe shingoni mwake. Ndipo akaombewa, naye Roho Mtakatifu alikuwa ametangaza amepona.

15 Vema, alipoenda nyumbani, alisema, "Vema, labda nitaenda tu na kula sasa, niko sawa." Kwa hiyo akaanza kula, ndipo ikamfanya mgonjwa sana. Kisha majuma matatu au manne yakapita, na bado, angejaribu kuwa na imani ya kusonga mbele.

16 Ndipo mumewe akamwambia, kasema, "Mpenzi, sijali wewe kuwa na imani kama hiyo," lakini kasema, "unaleta tu shutuma juu ya huduma yenyewe ya Kristo." Jinsi mume huyo alivyokuwa na ufahamu duni! Yeye hawezi kufanya hivyo maadamu anakiri Neno Lake, kwa kuwa Yeye ni Kuhani Mkuu wa maungamo yetu. Hawezi kutufanyia jambo moja mpaka kwanza tukiri limefanywa.

17 Ninyi watu ambao mmeokoka, mnajua jambo hili. Mngeweza kuja pale madhabahuni na kulia, na kujilaza madhabahuni na kukiri, na, yote utakayo, na kulia, na kuomba, na kupigapiga madhabahuni mwaka baada ya mwaka, wala kamwe hamtaokolewa mpaka mtakapokubali msamaha Wake. Mnaona? Ni kitu fulani unachokubali, ni chako, ni mali yako. Uponyaji ni wako, huna budi kuukubali. Na mpaka utakapoukubali . . .

18 Kitabu cha Waebrania kinasema Yeye ni Kuhani Mkuu wa kukiri kwetu, ama maungamo yetu, yote mawili yamefasiriwa vivyo hivyo. Tunapoungama, Yeye ni Kuhani Mkuu kufanya upatanisho juu ya yale tunayokiri, nasi tunaikiri kazi Yake iliyomalizika pale Kalvari.

19 Mwanamke huyu alikuwa akifanya hivyo. Asubuhi moja alikuwa akiosha vyombo vyake, na mara, kasema alikuwa akiwazia juu ya ule mkutano, naye mumewe alikuwa amemwambia usiku uliotangulia, kasema, "Mpenzi, ninaamini afadhali uendelee kufuata mlo wako kikamilifu, na kadhalika, na uache kusema kuhusu kuponywa." Kasema, "Huenda akakuponya siku moja."

20 Akasema, "Mume wangu, kama mtu huyo angeweza kuniambia mambo ambayo nimefanya maishani mwangu, naye alikuwa sahihi, naye akaniambia, BWANA ASEMA HIVI, nimeponywa, nitaamini hilo mpaka nitakapokufa." Hiyo ndiyo njia. Kasema, "Kama alitangulia kuona kile nilichokuwa, nilichokuwa nimefanya, hakika anaweza kuniambia kile ningefanya."

21 Ndipo mumewe akaenda kazini, naye alikuwa akiosha, alisema, vyombo, naye akahisi hisia baridi kidogo ikimpiga. Akashangaa, "Ni kitu gani hicho?"

22 Akashikwa na njaa sana, na baada ya kushikwa na njaa, akawazia, "Sina budi kula kipande cha tosti." Akachukua tosti kidogo na kuila, kwa kawaida alianza kutapika, ilikuwa ni kidonda cha duodeni, angetapika, bali ha—hakutapika.

23 Ndipo baadhi ya watoto walikuwa wameacha kwenye sahani zao, mnajua jinsi mama atakavyokuwa, kutoka kwa watoto wao, uji wa shayiri. Na huo ulimchoma sana wakati angeunywa huo uji wa shayiri, halafu, wanga, na kadhalika, wakati alipokula vijiko vichache vyake, havikumsumbua, kwa hiyo basi akanywa uji wote wa shayiri uliosalia kwenye sahani, haukumsumbua, kwa hiyo akajikaangia nyama kidogo ya nguruwe na mayai, naye akawa na yubile ya ulaji bora, kisha akanywa kikombe kikubwa cha kahawa, naye alikuwa tu na wakati mzuri sana.

24 Na baada ya kitambo kidogo, akangoja kwa saa kadhaa na kila kitu kilikuwa sawa, ndipo akajisikia vizuri sana, alikuwa akikimbia huku na huko akipiga mayowe, akashuka mbio barabarani kumwambia jirani yake. Basi alipofika kule chini, ilikuwa yapata saa tatu na nusu au saa nne, jirani yake alikuwa amesimama sakafuni akipiga mayowe, naye alidhani mtu fulani alifia mle. Kwa hiyo akaingia mbio, nao wote wawili wakakumbatiana. Naye jirani yake alikuwa na shuka mkononi mwake.

Kasema, "Unafanya nini na hilo shuka?"

Kasema, "Ninajaribu kutafuta kitu hicho kilichotoka kooni mwangu muda mfupi tu uliopita, kabla sijaamka." Akasema, "Mahali pale palipotoka kooni mwangu."

25 Nao wakaendesha, nadhani ilikuwa kama maili mia tatu kufika kwenye mkutano, ama zaidi, ku—kusimulia hilo tukio. Hilo ni moja kati ya maelfu.

26 Ilikuwa ni kitu gani? Malaika yule yule wa Bwana anayejua yaliyokuwako, na kubashiri yatakayokuwako, Yeye sikuzote hawezi kuja kukuokoa katika sekunde moja, hawa makasisi wanajua hilo, Danieli aliomba, na siku ishirini na moja kabla Malaika hajaweza kumfikia, bali alikuwa amepitia kwenye ujirani akithibitisha Neno, nao walikuwa wazima.

27 Sasa, hivyo ndivyo ilivyo. Hatuna budi kukumbuka ya kwamba uponyaji ni kazi iliyomalizika pale Kalvari, na jambo pekee ambalo mtu yeyote anaweza kufanya . . .

28 Sasa, mhudumu ambaye amefundishwa katika Neno, anaweza kusimama na kuwahubiria Neno. Sasa, kama akihubiri Neno, "Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu." Hilo—hilo ndilo la asili.

29 Lakini basi Mungu ni Mungu mwema, kama rafiki yetu mwema Ndugu Oral Roberts anavyolielezea. Yeye ni Mungu mwema. Halafu basi, hata hivyo tusipoliamini Neno Lake kwa ajili yake, basi isitoshe, tusipolichukua Neno Lake, Yeye ana njia nyingine. Yeye atatuma, Yeye ana karama kanisani, kuna karama tisa za kiroho zilizowekwa mahali hapo, kila kusanyiko la mahali hapo, zinapaswa kufanya kazi kikamilifu katika kila kusanyiko, kila kanisa. Na katika hizo kuna karama za lugha na kufasiri lugha.

30 Na sasa, huko si kurudia jambo fulani, ama kurudia-rudia bure, ni kusema jambo fulani moja kwa moja lipate kufasiriwa kwa mtu fulani katika kusanyiko hilo, ama kitu fulani, kufanya njia. Lugha, zinapofasiriwa, ni unabii, na ni tamshi la kinabii linalotolewa kwa watu ku—kuwaambia la kufanya, ama kitu fulani cha kuwasahihisha. Loo, laiti kanisa kuu la Mungu aliye hai lingeweza tu kuwekwa katika utaratibu! Ninaona ni . . .

31 Halafu mbali na hayo, Yeye ana ofisi tano za huduma. Kwanza ni mitume ama wamishenari, neno *mtume* linamaanisha "mtu aliyetumwa," *mmishenari* linamaanisha "mtu aliyetumwa." Pili, manabii, wainjilisti, wachungaji, na kadhalika, hizo ni karama zilizotolewa na Mungu ambazo zimewekwa kanisani, zimechaguliwa tangu zamani na Mungu na kuwekwa kanisani. Huwezi kujifanya mwenyewe mhudumu, wewe . . . Mungu hana budi kukuita kuwa mhudumu. Manabii wamekusudiwa tangu zamani, wao ni manabii.

32 Sasa, kuna karama ya unabii kanisani, hiyo ingeweza kuwa juu ya mmoja, halafu mwingine, mwingine, mwingine, na kadhalika, ya unabii; Paulo alisema nyote mnaweza kutoa unabii mmoja mmoja.

33 Lakini kuna tofauti kubwa kati ya nabii na unabii. Unabii hauna budi kupambanuliwa na mashahidi watatu, wawili au watatu, kabla haujatolewa ama kukubalika kanisani, kulingana na Maandiko, bali nabii, kama vile nabii wa Agano la Kale, walikuwa na Neno la Bwana, kule kuhamishwa kulikuwa kweli kwao. Nao walijulikana, kwa sababu Biblia ilisema, "Akiwapo miongoni mwenu mtu wa kiroho au nabii, Mimi Bwana, nitajitambulisha Mwenyewe kwake, nitasema naye katika maono, na kujifunua Mwenyewe katika ndoto. Na kama yale mtu huyu asemayo yakitimia, basi msikieni, kwa kuwa niko pamoja naye. Yasipotimia, basi msimsikie, siko pamoja naye, msimwogope."

34 Sasa, mnaona, kwa hiyo uponyaji huo wa Kiungu ni jambo ambalo Kristo alitufanyia. Sasa, hatuna budi kuwa na imani.

35 Sasa, ninakuta matabaka mawili ya watu katika safari yangu, moja ni la kimsingi, hilo lingine ni la Kipentekoste. Sasa, wa kimsingi wanajua kile walicho kimahali, bali hawaingii

ndani vya kutosha. Wanajua kimahali kwamba wao ni wana wa Mungu, bali hawaingii ndani vya kutosha.

36 Kama nilivyowazia juu ya Ndugu yetu mpendwa Billy Graham wakati alipokuwa katika mji wetu, nilikutana naye mara kadhaa na tulikuwa kwenye kiamshakinywa chake cha wahudumu, ndipo akasema, "Paulo aliingia mjini na kuhubiri Injili, ndipo mtu mmoja akaongoka, akarudi mwaka mmoja baadaye," kasema, "alikuwa na waongofu thelathini kutokana na huyo mmoja." Kasema, "Nitaingia mjini na kukaa majuma sita, na kupata elfu ishirini, nirudi katika miezi mingine sita wala nisingeweza kupata ishirini." Akasema, "Kuna nini? Ni nyinyi wahubiri wavivu," akasema, "mnaketi huku mmeweka miguu yenu juu ya dawati, badala ya kutoka nje na kuwatembelea."

37 Sasa, huyo mwinjilisti alikuwa na kitu fulani hapo, bali hakuwa na yote. Ni nani aliyemchukua huyo wa Paulo? Paulo alimwingiza ndani vya kutosha katika Kristo mpaka akajazwa na Roho Mtakatifu, basi alikuwa akiwaka moto hata angeweza kuuwasha moto mji mzima. Lakini mnapowaomba tu wasimame, wamkubali Kristo kama Mwokozi, kisha warudi waketi chini, hawajaingia ndani vya kutosha kujua la kufanya. Huna budi kuwaingiza katika ubatizo wa Roho.

38 Kwa hiyo ninaona watu wa kimsingi, kimsingi wanajijua kuwa wao ni nani, bali hawana imani, ndipo ninawaona Wapentekoste ambao wana imani nyingi, bali hawajui wao ni akina nani. Ni kama tu mtu, mtu mmoja ana pesa kwenye benki lakini hawezi kuandika hundi, na huyo mwingine anaweza kuandika hundi ila hana pesa kwenye benki. Kama ungeweza kuwaleta hao pamoja, Injili ingeleta faida kubwa. Hiyo ni kweli. Weka mafundisho kidogo ya kimsingi katika kanisa la Kipentekoste, ama imani ya Kipentekoste katika mikutano ya kimsingi.

39 Unaona, inakubidi kujua kimahali, kwanza, Kristo, mahali unaposimama. Wewe ni mrithi wa hii, ni mali yako binafsi, ni yako, ni zawadi ya Mungu kwako. Hakuna mtu anayeweza kuiondoa kwako, ni yako. "Mtakalomwomba Baba katika Jina Langu, hilo nitalifanya." Ni nani anayeweza kukana chochote hapo? "Amin, amin, nawaambia, ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka,' usiwe na shaka moyoni mwako bali uamini ya kwamba yale uliyosema yatatimia, yatakuwa yako yale uliyosema." Ni ahadi za jinsi gani! Sio tu kwa uponyaji, bali kwa chochote kile.

40 Sasa, huna budi kujua lengo lako, na nia yako, halafu mapenzi ya Mungu. Iwapo ni mapenzi ya Mungu, na nia yako ni sahihi, na lengo lako ni sahihi, basi huo mlima utaporomoka. Lakini nje ya hayo, ungeweza kupiga mayowe mpaka ukapwelewa na sauti na ukafa, na kamwe usingesogea.

Unaona? Ninii yako . . . Jambo la kwanza, haina budi kuwa ni mapenzi ya Mungu; jambo lingine, ni kusudi lako katika kwenda na kulitekeleza; halafu lengo ulilo nalo. Unataka kuwa mtu mkubwa . . .

41 Kuna kitu kimoja ambacho—ambacho Yesu Kristo alipungukiwa wakati alipokuwa duniani, hicho kilikuwa ni maonyesho, Yeye hakuwa mtu wa maonyesho. Usingeweza kusema Yeye ana majivuno, Yeye alijitenga, mnyenyekevu. Aliidhibiti mikutano Yake kusudi aweze kwenda popote Baba alipomwongoza kwenda. Ndipo mmoja wa ndugu Zake akasema, "Kama unaweza kufanya mambo haya, kwa nini usije kwa Kayafa? Ingia miongoni mwa watu mashuhuri sana na marabi na ufanye hivyo, ili kila mtu aweze kukuona Wewe. Unafanya nini ukiambatana na kundi la watakatifu wanaojibingirisha ama . . .?" Sasa, sikumaanisha hilo namna hiyo, nilimaanisha wavuvi, na kadhalika. Mimi, vema, nilikuwa tu nikiwazia yale mmoja wa ndugu wa lile kanisa ambalo ndio kwanza nitoke alisema.

42 Vema, ndivyo hivyo, mnaona, bali Kristo hakuwa wa maonyesho, Yeye alisema, "Wakati wenu ni sikuzote." Hiyo ni kweli.

43 "Alikuja kwa walio Wake, wala walio Wake hawakumpokea." Hilo ndilo jambo la kuhuzunisha sana nijualo katika Maandiko. "Alikuja kwa walio Wake, wala walio Wake hawakumpokea."

44 Sasa, tunapolikaribia Neno usiku wa leo, ninawatakeni mkumbuke hilo, ya kwamba sisi . . . mtu ambaye . . . Kumbukeni, ya kwamba Mungu hana wenye kiburi. Unapofikia mahali ambapo uko tayari kuwa si chochote, basi Mungu anaweza kufanya kitu kutoka kwako. Lakini maadamu unajaribu kuwa mkubwa, na matangazo mengi ya kuvutia, na upuuzi huu wote, na kuendelea, maoni yangu, jambo fulani limetukia. Mnaona?

45 Yesu alienda akitenda mema, akiwaendea maskini na wahitaji, Yeye kamwe hakujipatia Mwenyewe sifa yoyote. Mliwahi kuwazia hilo? Hakujipatia Mwenyewe sifa yoyote. Mtu aliyetengeneza jino bandia alijipatia mwenyewe sifa, lakini Yule aliyeumba jino halisi hakujipatia Mwenyewe sifa. Mtu aliyetengeneza mkono bandia alijipatia mwenyewe sifa, bali yule Mtu aliyeumba mkono halisi hakujipatia Mwenyewe sifa. Njia ya kupanda juu ni kushuka, daima kumbukeni hilo. Iweni wanyenyekevu, iweni wazuri na wema, iweni waumbaji, acheni Kristo awe ndani yenu.

46 Je, umewahi kuona watu unaopenda kuwa karibu nao, unapenda tu kuwa karibu nao? Kwa sababu wanaumba mazingira, ya Kimbinguni, nawe unapenda kuwa karibu nao. Wengine wanaonekana kuwa ni watu wazuri, lakini unaninii tu, sina budi kuondoka mara moja moja, ambapo . . . Mnajua

ninalomaanisha. Na hata hivyo wanaonekana kuwa watu wazuri, si waumbaji.

47 Naye mwanadamu alifanywa kuwa mungu, tunajua hilo. Mwanzo 1:26, alikuwa na mamlaka juu ya dunia nzima, naye alifanywa kuwa mungu mdogo. Na sasa, anapompokea Mungu, anakuwa mwana wa Mungu tena. Aliumbwa kwa mfano wa Mungu. Mungu alikuwa na mikono, Mungu alikuwa na miguu, na kwa hiyo basi mwanadamu aliumbwa kama Yeye, kwa hiyo yeye ni mungu mdogo. Lakini dhambi imepofusha kila mshipa mwilini mwake, niani mwake, moyoni mwake. Lakini sasa, kamwe usijaribu kulichambua, huwezi kulielewa.

48 Katika bustani ya Edeni Shetani alichagua sehemu yake ya mwanadamu, kichwa chake, akili zake; Mungu akauchukua moyo wake. Wasomi watahoji, "Kwa nini? Vema, niko—niko *hivi*, na niko *vile*." Kamwe hutafika popote pamoja na Mungu hapo. Lakini moyo wako, imani yako itakufanya uamini mambo ambayo akili yako haijui chochote juu yake, tupilia mbali hoja. Unaona, lazima uwe na hakika, nawe ukae hapo mpaka utakapokuwa na hakika, basi wakati ukiwa na hakika, hakuna kitu kinachoweza kukugeuza.

49 Sasa, hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu kabla hatujamkaribia Mwa—Mwandishi wa Neno hili, tunapolisoma. Nami nashangaa usiku wa leo, huku vichwa vyetu vimeinamishwa na macho yetu yamefumbwa, kuna yeyote hapa ambaye angetaka kukumbukwa katika maombi? Basi acha ijulikane kwa mkono wako ulioinuliwa. Ungesema, "Bwana, ninakuhitaji, ninakuhitaji kwa ajili ya afya yangu, ninakuhitaji kwa ajili ya nafsi yangu." Mungu awabariki. Mungu awabariki. Hilo ni jema. "Baba, niongoze, ninahitaji Roho Wako aongozaye."

50 Baba yetu wa Mbinguni, tunapokaribia tena katika Jina la Bwana Yesu, ulisema kwamba tuombe kwa wingi furaha zetu zitimie. Sasa, tunakuja kuomba rehema, kwanza, kwa ajili ya dhambi zetu wenyewe, mambo ambayo tumewazia na kufanya ambayo yalikuwa kinyume na uongozi Wako, tunaomba ya kwamba utusamehe.

51 Na tunaposimama hapa katika madhabahu hii takatifu, ambapo Roho Mtakatifu yupo, na, loo, jinsi ambavyo mara nyingi nimeshangaa jinsi ningejisikia kama ningeweza kushikilia katika bilauri matone mawili tu ya Damu Yake halisi. Jinsi ningeyashikilia kifuani mwangu na kulia, kwa sababu ninajua ya kwamba ilikuwa ni ile Damu ambayo iliniokoa! Lakini, usiku wa leo, Wewe umenipa kilicho kikubwa kuliko hiyo, wale hasa walionunuliwa kwa Damu Yake ili kuwazungumzia. "Kwa maana aliupenda ulimwengu sana hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asiangamie, bali awe na Uzima wa Milele." Sasa, Yeye aliwazia

zaidi juu ya watu Wake kuliko alivyowazia juu ya Damu Yake Mwenyewe, kwa hiyo akatoa Damu Yake apate kulinunua kanisa hili. Nami hapa nimesimama usiku wa leo kulifundisha kanisa hili njia za Uzima.

52 Loo, Baba mwenye rehema, hakuna mtu anayestahili kufanya hivyo. Tunaomba, Bwana, ya kwamba utusamehe. Na kama ulikuwa unamtafuta mtu anayestahili, ungewapata wapi? Hatuna yeyote, sisi sote ni wachafu, Baba. Lakini uturehemu kwa sababu ya ahadi Yako ambayo ulisema utafanya hivyo, ulisema, "Mimi ni Mzabibu, ninyi ni matawi," na kama tukikaa ndani Yako, kwamba tunaweza kuomba tutakalo, na tutapewa. Ulisema, "Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya, hata kubwa kuliko hizi, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba Yangu." Sasa, kusudi Neno Lako lipate kutimizwa usiku wa leo, Bwana, ninaomba ya kwamba utadhihirisha Uwepo Wako miongoni mwetu kwa njia isiyo ya kawaida.

53 Ninawaombea wale walioinua mikono yao, Baba, Mungu, uturehemu. Na pia ninaomba dua tena kwa ajili ya maskini msichana mdogo, kipofu, aliyesimama ukumbini usiku wa leo, alitaka kurudi kwa watu wake, apate kuwa mmishenari. Ee Mungu, jalia mtoto huyo afunguliwe macho.

54 Ninamwombea yule ndugu wa thamani kule hospitalini, ni wa First Assembly of God hapa mjini, yuafa. Ee Mungu, uzuie mkono wa mauti wakati kanisa hili, mwili huu, ukiomba rehema. Usikie Mungu na Baba mkuu, unayejibu maombi.

55 Tungeomba kwa ajili ya kila mmoja wetu hapa, kuomba kwa ajili ya maskini ndugu yetu mchungaji, na kwa ajili ya hawa wahudumu wengine, wainjilisti, na—na watumishi Wako walio jukwaani, wavuvie, Bwana, na uipe huduma yao msukumo mkuu wa Roho Wako Mtakatifu.

56 Jalia nyumba hii ndogo hapa tuliyomo usiku wa leo iwe wazi mpaka Yesu atakapokuja. Kama akikawia, wamishenari na wahudumu na watumwe kutoka hapa kwenda kote ulimwenguni. Na iwe kweli nyumba iliyo kando ya barabara ambamo mchovu anaweza kuingia na kupata raha.

57 Waokoe waliopotea, waponye wagonjwa, watakase waaminio, na utupe imani usiku wa leo, Baba. Ee Mungu, hiyo ndiyo tunayohitaji, imani katika Neno Lako. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

58 Katika Yohana Mtakatifu 12:20:

> *Palikuwa na Wayunani kadha wa kadha miongoni mwa watu waliokwea kwenda* kuabudu kwenye sikukuu*:*
>
> *Hao walimwendea . . . Filipo, mtu wa Bethsaida ya Galilaya, wakamwambia, wakisema, Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu.*

59 Basi somo langu linapatikana, Waebrania 13:8:

*Yesu Kristo yeye yule jana, . . . leo, na hata milele.*

Sasa, ili nisiwacheleweshe, bali kusudi nipate usikivu wenu kwa dakika chache kujenga imani karibu na kila mmoja wenu mpate kuponywa.

60 Basi ninapoliangalia kanisa usiku wa leo, ninamwona mtu hapa akikohoa, kipenzi kimelala pale, kitoto kichanga cha thamani cha mama fulani akiwa na kichwa kikubwa kilichojawa maji, kikifa, mpendwa mwanamke mkongwe aliyeketi kwenye kiti cha magurudumu, na kadhalika. Loo, laiti kungekuwa na njia fulani, jambo ambalo ningeweza kufanya! Mnaona?

61 Na labda hawa kwenye kiti cha magurudumu, na kadhalika, wangeishi maisha ya kawaida, na labda mwanamume ama mwanamke mzuri, anayeonekana mwenye afya aliyeketi huko nje, kijana, atakuwa amekufa kufikia kesho kwa mshtuko wa moyo. Mnaona? Hawa huenda wakaishi muda mrefu kuliko wao, hatujui. Naona fimbo nyeupe za watu, vipofu wakitembea, loo, laiti kungalikuwa na kitu ninachoweza kufanya kuwasaidia! Kama sikuwazia ningeweza kuwasaidia, kamwe nisingepitia hapa. Kama sikufikiri ningeweza kuwasaidia hawa watu . . .

62 Si kwa ajili ya pesa, hizo sizichukui. Nami ni—nina umri wa miaka hamsini na mmoja, nimekuwa nikihubiri kwa muda wa miaka thelathini na mmoja wala sijawahi kuchukua sadaka maishani mwangu mwote. Kwa hiyo, si—si sininii . . . Hutuzihusishi pesa kwake. Tunaifanya mikutano yetu midogo ili isitubidi kuwa na mipango mikubwa na kadhalika ya kuendesha ili tuweze kwenda kwenye kanisa dogo kuliko yote, ama popote Bwana aongozapo, huko ndiko tuendako.

63 Sasa, siwahukumu ndugu walio na vipindi hivyo vikubwa, na matangazo ya televisheni, na kadhalika, hilo ni sawa. Ninamshukuru Mungu kwamba kuna watu ulimwenguni ambao Yeye anaweza kuwaaminia pesa kama hizo, wanaoweza kuzistahimili. Lakini kwangu mimi, kamwe ni—nisingeweza kufanya hivyo, ingenibidi kuchukua pesa, wala si—sijapata kufanya hivyo bado, nami ninaomba Mungu atanisaidia kwamba haitanilazimu kamwe.

64 Kwa hiyo niko hapa kuwasaidia. Na kama sikufikiri ningeweza kuwasaidia, hakika nisingekuwa hapa, ningekuwa nyumbani usiku wa leo pamoja na mke wangu, na mvulana mdogo, na wasichana wawili wadogo. Ningekuwa nimeketi huko karibu na moto mahali fulani usiku wa leo huko mashariki, nikifurahia pamoja nao. Lakini mimi karibu ni mgeni kwao, ninawaona tu mara moja moja, nikisafiri kote ulimwenguni.

65 Lakini, kulikuwa na swali lililoulizwa hapa katika Maandiko. Na asubuhi ya leo nilikatiza kuzungumza juu ya neno la *Matarajio*, kutarajia. Sasa, ninatumaini ya kwamba ulienda nayo nyumbani, na kuyachunguza Maandiko yote

upate kujua la kutarajia. Neno la Mungu linatwambia kile tunachoweza kutarajia.

66 Na kama tukilipokea Neno hili bila shaka yoyote kuchanganywa ndani yake, tutapokea kile kilichotuleta hapa. Lakini ukiondoka ukisema, "Vema sasa, kama tu ilivyotarajiwa, si—sikuninii . . ." Vema, hutaona chochote. Lakini kama ukija ukitarajia kumwona Bwana Yesu akijidhihirisha Mwenyewe miongoni mwa watu, utaondoka umeridhika. Hakika utaridhika. Utajua ya kwamba jambo fulani lilitukia.

67 Lakini ukisema, "Vema, mimi . . . kama tu nilivyotarajia, mwingine tu, loo, mwinjilisti anayesimama akinena," na—na hiyo, basi hiyo ndiyo yote utakayopata. Kwa kawaida unapata kile unachotafuta.

68 Kwa hiyo fungua moyo wako usiku wa leo, na ushushe mwavuli, na ninii tu, loo, ulipokee tu, Mungu moyoni mwako. Kisha mwondoke, mrudi makanisani mwenu popote mnapotoka na mkamwambie mchungaji wenu kwamba kweli Bwana Yesu ndiye Mponyaji mkuu, ya kwamba Yeye Ndiye anayemwokoa na kumjaza mwaminio kwa Roho Wake, na kumfanya kiumbe kipya katika Kristo. Mchungaji aseme, "Unajuaje hilo?"

Useme, "Ninao ujuzi, najua."

69 Ndugu fulani si muda mrefu uliopita ambaye hakubali kwamba Kristo ni Mponyaji, anamfanya Yeye Mungu fulani wa kihistoria, alisema, "Loo, siamini! Lolote lingetukia," kasema, "bado siamini katika uponyaji wa Kiungu."

70 Nikasema, "La, hasha, haukuwa kwa ajili yako. Haukuwa kwa ajili ya wasioamini, ulikuwa ni kwa ajili ya wale wanaoamini, ulikusudiwa tu kwa ajili ya waaminio." Kwamba, Yeye—Yeye hakununua uponyaji we—wetu kwa ajili ya wasioamini, aliwanunulia wale wanaoamini. Ahadi hiyo si kwa wasioamini, bali kwa hao waaminio.

71 Kwa hiyo Wayunani hawa wakaja kwenye karamu. Sasa, Wayunani walikuwa watu wenye elimu, nao walikuja kwenye Sikukuu hii ya Pentekoste ku—kuabudu, ndipo walipokuwa hekaluni walikuwa wamesikia habari za Bwana Yesu. Na kwa *namna fulani*, siamini ya kwamba kuna mtu yeyote anayeweza kusikia Jina hilo la kupendeza likiitwa kamwe, ila ambaye angetamani kumwona. Unaposikia habari za Yesu, kuna kitu fulani kuhusu hilo Jina la Bwana Yesu ambacho—ambacho huvuvia, wala kamwe huwezi kujisikia vivyo hivyo. Ni Jina lipitalo majina yote.

72 Alishuka kutoka Mbinguni, nao ulimwengu ukampa jina duni kuliko yote yaliyokuwamo duniani, Beelzebuli, mpiga ramli, ibilisi. Ndipo akaenda kwenye mji duni kuliko yote duniani, Yeriko, naye alikuwa duni sana hata mtu aliye mfupi kuliko wote mjini ilimbidi kuchungulia chini apate kumwona, Zakayo. Lakini alipolipa gharama ya ukombozi, Mungu alimpa

Jina lililo juu ya kila jina. Hata jamaa yote Mbinguni na duniani inaitwa Yesu. Naye alikiinua Kiti Chake cha Enzi juu sana, hata inambidi kuangalia chini apate kuona Mbingu. Hiyo ndiyo tofauti, jinsi ulimwengu ulivyomtendea, na vile Baba alivyomtendea wakati alipokuja.

73 Sasa, basi hawa Wayunani walikuwa wadadisi, nao walikuwa wamesikia habari Zake, walisikia juu ya kazi Zake kuu. Basi kupitia, labda, udadisi, ama labda kwa manufaa maaminifu, walikuja na kusema, "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu."

74 Nami ninaamini kama ningeweza kufafanua nia ya kanisa hili usiku wa leo, watu hawa, hiyo ndiyo shauku ya moyo wetu. Ni wangapi hapa wangetaka kumwona Yesu? Hakika. Vema basi, nitawaulizeni swali: Je, wa—waliweza kumwona Yeye? Naam, bwana. Filipo aliwapeleka kumwona, akawapeleka kwa mmoja wa hao ndugu, nao wakawapeleka kumwona Yesu.

75 Kwa hiyo kama waliuliza, na kutamani kumwona Yesu, walipewa majaliwa ya kumwona na mmoja wa watumishi Wake. Sasa, na kama Waebrania 13:8 ni Maandiko yaliyovuviwa vizuri, yaliyosema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele," basi kama hiyo ndiyo shauku yetu, basi kwa nini hatuwezi kumwona?

76 Sasa, hamna budi kukumbuka Neno hili ama ni Kweli au si la kweli. Hakuna kuhitilafiana ndani Yake. Nami nimemwahidi mtu yeyote, ninapata dola mia moja kwa juma, nami na—namwahidi mtu yeyote mshahara wa mwaka mmoja anayeweza kunionyesha kuhitilafiana katika Neno ambayo haliinyooshi kabisa, hakuna.

77 "Limefichwa kutoka kwa macho ya wenye hekima na akili, na kufunuliwa watoto wachanga watakaojifunza." Yesu alimshukuru Baba kwa kufanya hivyo. Neno halichanganyikiwi, watu ndio waliochanganyikiwa, si Neno. Kwa hiyo Roho Mtakatifu aliandika Neno, inahitaji Roho Mtakatifu kulifasiri Neno, nalo lote litafanya kazi sawasawa kabisa.

78 Sasa, kama Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, na Mungu anisamehe kwa kusema *kama*, kwa sababu linasikika la kukufuru, Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele, vema basi, kama mnatamani kumwona, basi kwa nini msiweze kumwona? Sisi ni watumishi Wake, basi ni kwa nini hamwezi kumwona? Je, mngetaka kufanya hivyo? Mngependa kumwona? Vema.

79 Ninaamini ya kwamba Yeye alitoa ahadi hii kwamba "Walipo wawili watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, hapo nitakuwa katikati yao." Sasa, hiyo ni kweli? Sasa, kama hiyo si kweli, basi Biblia si ya kweli, na wokovu wako si wa kweli, nasi tumepotea na wenye mashaka, kati ya watu wote, sisi ndio wenye mashaka zaidi, kwa sababu tuna ki—kitu cha bandia

tunachowazia juu ya Kristo anayekuja, na Mbingu ya kuendea, wala hakuna kitu kama hicho.

80 Vema, kama Neno hili si la kweli, basi Neno hilo ni Yeye, na basi yote ni ya uongo, lakini kama ni kweli, basi kila Neno Lake ni la kweli. Si mengine kwa wakati mmoja, mengine kwa mwingine, wakati wote ni lile lile, ambapo Yeye anaweza kuwapata waaminio.

81 Sasa, kama Yesu atakuja kwenye kusanyiko hili usiku wa leo, linaloonekana . . . Sasa, Yeye asingeweza kuja katika mwili wa kawaida, kwa sababu huo umeketi kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, bali Yeye anaweza kuingia humu ndani kwa Roho Mtakatifu, na kuwaonyesha Mwenyewe yuko hapa, akifanya kazi katika kanisa Lake. Mnaamini hilo? Hana budi kuwa ninii, kila kitu katika kanuni ile ile, hana budi kuwa na upendo ule ule, huruma zile zile, kazi zile zile, dhihirisho lile lile, ikiwa Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.

82 Sasa, kumbukeni, Yesu, wakati kazi zilipokuwa zikifanywa, Yesu hakumponya mtu yeyote, alisema, "Siwezi kumponya mtu yeyote." Alisema, "Si Mimi nizitendaye hizo kazi, ni Baba Yangu, Naye anakaa ndani Yangu." Hiyo ni kweli? "Anakaa ndani Yangu. Na kitambo kidogo," alipoondoka, Yeye alisema, "na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa Mimi," *Mimi* ni kiwakilishi nafsi, "nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari," mpaka ulimwengu utakapofikia mwisho, *Mimi*. "Na kazi nizifanyazo ninyi nanyi mtazifanya. Mkikaa ndani Yangu na kazi Zangu ndani yenu, ombeni mtakalo, nanyi mtapewa." Loo, ahadi hizo kuu, jinsi zinavyoifurahisha nafsi yangu!

83 Katika siku ambapo makombora ya atomiki, Warusi wana sputniki hewani, na haya yote, mbona, hakuna raha popote, ila katika Kristo. Hakuna kitu kimoja, taifa letu, hatuwezi kujenga matumaini yetu juu yake, kwa sababu taifa lolote dogo lingeweza kutupa bomu hapa na kutulipulia mbali kutoka duniani. Mambo ya vita yako karibu kwisha, unahitaji tu mtu mmoja kuvuta wenzo, wote utavunjika vipandevipande.

Nasi tunaona huwezi kujenga matumaini yako juu ya kitu kingine ila Kitu kimoja, nami ninamnukuu Eddie Perronet hapa aliposema:

> Nyote zisifuni nguvu za Jina la Yesu!
> Malaika na wasujudu;
> Leteni taji ya kifalme,
> Na kumtawaza kuwa Bwana wa wote.
>
> Kwa kuwa juu ya Kristo, Mwamba imara, ninasimama;
> Ardhi nyingine yote ni mchanga udidimiao,
> Ardhi nyingine yote ni mchanga udidimiao.

84 Tumaini letu la pekee. . .Wanajaribu kuchimba shimo chini ardhini, watambae ndani yake. Wana bomu litakalolipua shi—shimo ardhini lenye kina cha futi mia tano, na karibu maili mia moja mraba. Vema, kama wewe ulikuwa futi elfu kumi chini ya dunia, lingevunja kila mfupa mwilini mwako, mtikiso wake.

85 Lakini kuna kimbilio, loo, halijatengenezwa kwa felisi, bali limetengenezwa kwa manyoya, chini ya mbawa Zake. Loo, napenda kimbilio hilo, kudumu humo kwa amani, utamu, nikijua hili, kwamba mara tu. . .kabla bomu hilo halijapigiwa filimbi ya kuanza, kwa mbawa Zake atatuinua juu. Loo, hilo ndilo ninalotazamia, huko Kunyakuliwa kukuu, na kukaribia kwa Bwana wetu Yesu. Na kukuona kukikaribia sana, mioyo yetu inaruka tu kwa furaha, kujua kwamba, ni furaha.

86 Mtu fulani alisema, "Ndugu Branham," kasema, "unawatisha watu kwa kuwaambia Bwana Yesu yuaja, mwisho wa ulimwengu."

Nikasema, "Loo, jamani, sio Wakristo, loo, bila shaka sio."

87 Paulo alisema, "Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, imani nimeilinda, na baada ya hayo nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana, Hakimu mwenye haki, atanipa siku hiyo, na si mimi tu, bali na wale wote wanaopenda kuonekana Kwake."

88 Loo, ni—ni jambo gani kubwa zaidi lingeweza kutukia kuliko kuja kwa Yesu sasa hivi? Bila shaka. Majaribu yetu yatakwisha. Tuendeleeni tu kushikilia mpaka atakapofika hapa, tukifanya kazi, tukiuhifadhi wakati, na kufanya kila dakika iwe na maana Kwake. Popote tulipo, tuseme neno dogo kwa ajili Yake.

89 Sasa, kama Yeye amekuwa halisi sana kwetu, nasi tumeona rehema Yake na kuona kile alichokuwa, sasa, nasi tuko chini ya matarajio ya kumwona usiku wa leo, basi kwa nini hatuwezi kumwona? Nitawaambia, Yeye yuko kila mahali kama mkiangalia tu kote, shida yake ni kwamba watu hawaangalii kote kutosha kumwona Yeye.

90 Tunaishi kwenye Mto Ohio, na, loo, ni mahali pazuri pa kuvulia samaki. Kulikuwa na mvulana mdogo mjini mwetu aliyekuwa akicheza hapo chini mtoni pamoja na mzee mvuvi. Ndipo akamwuliza mama yake siku moja, walikuwa wafuasi wa kanisa moja kubwa mjini, akasema, "Mama, Mungu ni Mtu mkuu sana, kuna mtu yeyote anayeweza kumwona?"

Akasema, "Siwezi kukujibu hilo, Mwanangu." Kasema, "Mwulize mwalimu wako wa shule ya Jumapili."

Ndipo akamwuliza mwalimu wa shule ya Jumapili, naye akasema, "Sijui. Mwulize mchungaji."

Kwa hiyo akamwuliza mchungaji, naye mchungaji akasema, "La, mwanangu, hakuna mtu anayeweza kumwona Mungu na kuishi." Kasema, "Kamwe huwezi kumwona."

91 Haikumridhisha maskini mvulana huyo. Ndipo akashuka mtoni, na maskini mvuvi huyu, alikuwa ni shemasi kanisani mwangu, kwa hiyo a—alikuwa huko mtoni siku moja kwenye Kisiwa cha Maili Sita, akivua samaki. Basi walipokuwa wakienda zao, wakirudi kutoka mtoni, ikatokea dhoruba, nao iliwabidi kuweka kando chombo chao kidogo kwa dakika chache, dhoruba ikavuma.

92 Na huko Indiana na karibu na nchi za mashariki, ilipo miti migumu, mvua hiyo hunyesha na kuyafagilia mbali majani yote, ndipo upepo huo mdogo unavuma, wakati tu mpiga makasia anapoweza kujua, ncha ya makasia wakati inapogusa mawimbi hayo, ule muziki inaofanya juu ya hayo maji. Loo, si ajabu Roho wa Mungu alitembea juu ya maji kwanza. Kuona jinsi ambavyo . . .

93 Akishuka, maskini mvuvi huyu, maskini ndugu mzee aliyejazwa na Roho, akivuta makasia yake namna *hii*, na kusikiliza ncha ya makasia yake juu ya maji. Naye alikuwa akiangalia nyuma, akielekea, alikuwa akienda magharibi huku ameangalia mashariki, ndipo hapo upinde wa mvua ukatokea. Yule mzee, mwenzake alikuwa ameondoka, miaka mingi, naye alikuwa akiuangalia huo upinde wa mvua, ndipo juu ya ndevu zake za fedha kukatokea michirizi midogo ya machozi yakitiririka ndevuni mwake.

94 Maskini mvulana huyo mdogo aliyekuwa ameketi kwenye shetri ya hiyo mashua, akashikwa na shauku sana akakimbia mpaka katikati ya mtumbwi, naye akasema, akaangukia mikononi mwake, na kusema, "Bwana, nitakuuliza swali ambalo mama yangu, mwalimu wa shule ya Jumapili, wala mchungaji hawezi kuniridhisha." Akasema, "Je, mtu yeyote anaweza kumwona Mungu?"

95 Nalo likamzidia huyo mzee mvuvi, akavuta makasia ndani ya mtumbwi, akamkumbatia maskini mvulana huyo mikononi mwake, na kuzipapasa maskini nywele zake, na kusema, "Mungu aubariki maskini moyo wako, mwanangu, yote ambayo nimeona kwa miaka hamsini iliyopita imekuwa ni Mungu." Mwingi sana ndani, angeweza kumwona Yeye huko nje, kuona upinde wa mvua, popote ulipo. Hivyo ndivyo ilivyo.

96 Kama unamwangalia kwa mtazamo wa kiakili, kamwe hutamjua, huna budi kuangalia kupitia Kwake, umwache Yeye aingie ndani yako na kujionyesha Mwenyewe, Wake, kile Yeye alicho. Tunaweza kumwona Mungu kama tutaangalia tu kote. Nami ninahofia baadhi yetu huenda tukaangalia tumechelewa kupita kiasi.

97 Kulikuwa na mama mmoja katika duka la malimali huko Louisville, upande wa pili wa mto kutoka kwetu, miezi michache iliyopita, alikuwa na mvulana mdogo, alikuwa ni mvulana mdogo, yapata umri wa miaka mitatu. Nao watu

wakaona angezunguka-zunguka, achukue vitu, na kujaribu kumwonyesha, kutoka kwenye kaunta za maduka ya malimali. Naye alikodoa macho tu, huyo mvulana mdogo.

98 Kwa hiyo akaja kwenye kaunta nyingine, alikuwa ameanza kupagawa, ndipo akachukua kitu kingine, kama kile mvulana mdogo wa umri huo anachopaswa kuangalia, kisha akapiga kengele ndogo kwenye kipambo kidogo, kasema, "Angalia, Kipenzi! Angalia, Kipenzi!" Naye huyo mvulana mdogo aliketi tu amekodoa macho. Alikuwa amechoka, naye akaanguka tu juu ya kaunta, akipiga mayowe, "Loo, la, la, sivyo!"

99 Basi watu waliokuwa karibu wakamkimbilia huyo mama waone kilichotukia. Akasema, "Mvulana wangu mdogo, miezi michache iliyopita, alianza tu kukodoa macho moja kwa moja angani, hakuna kitu kinachopaswa kumvutia kinachouvutia usikivu wake." Kisha kasema, "Nilimpeleka kwa daktari, naye daktari akasema amepata nafuu, lakini," kasema, "sivyo." Kasema, "Yeye huketi tu na kukodoa macho, hataangalia vitu ambavyo anapaswa kuangalia kama mvulana mdogo wa umri wake."

100 Na jinsi hilo lilivyo kweli kwa kanisa siku hizi! Tumekuwa na watu mashuhuri wakivuka nchi hii kama Oral Roberts, na karama kuu zimeingia kanisani, nao, kanisa limeketi tu na kukodoa macho. Ubatizo wa Roho Mtakatifu umelishukia hili taifa, na makanisa mengi yamejazwa na Roho, na miamsho mikuu imetukia, nao ulimwengu unaketi tu na kukodoa macho angani. Mungu anapofanya jambo lolote, Yeye huwatarajia watu kuliangalia na kumwamini. Miujiza, na ishara, na maajabu ambayo Mungu hufanya ni kitu kidogo wanachotikisa mbele ya kanisa kuliamsha kanisa kwamba Yeye yuaja karibuni.

101 Mimi na mwanangu, hivi majuzi tulikuwa tumeizuru India, nami nikasoma makala kwenye gazeti tulilopata kwenye ndege, nayo ikasema, "Nadhani tetemeko la ardhi limekwisha." Siku chache kabla ya tetemeko la ardhi kuja . . .

102 Huko India wao huokota tu mawe na kujenga nyua, na kuta, na kadhalika. Hawana waya uliofumwa na vitu tulivyo navyo hapa, wao ni watu maskini sana. Milioni mia nne na sabini kule, na yapata, ilionekana kwangu, milioni mia nne wao ni ombaomba, na jambo la kusikitisha sana kuliona.

103 Baadhi ya ndugu wahudumu, kama ukipata kuona mionekano hiyo hu—huwezi kamwe kujisikia kuridhika hapa tena. Kuna kitu fulani, hao maelfu wakipiga mayowe na kulia wapate kusikia hadithi ya Yesu, na hapa inakubidi karibu uwashawishi watu waje kanisani. Lakini wao wana—wana njaa huko kwa ajili ya Mungu.

104 Nalo gazeti likaendelea kusema kwamba maskini ndege wote wanaotengeneza viota vyao kwenye nyufa za mawe, na kadhalika, waliruka wakaingia makondeni, wakaketi mitini.

Kisha kondoo wote na ng'ombe waliosimama karibu na kuta hizo kubwa wakaenda kondeni, na kuegemeana kwa karibu siku moja. Ndipo mara kukatokea tetemeko la ardhi na kuzitikisa na kuporomosha kuta hizo. Ndipo kwa siku moja maskini hao ndege walikaa mbali, nao ng'ombe wakakaa kondeni. Hatimaye, wakaanza kurudi karibu na kivuli tena, kwenye sehemu ya kuta zilizosalia.

105 Ilikuwa ni kitu gani? Mungu yeye yule ambaye angeweza kuwaita waingie safinani angeweza kuwaita waziondokee hizo kuta. Wangepoteza maisha yao kama wangalibaki kule.

106 Na kwa kweli iwapo Roho Mtakatifu angali anaweza kuwa na uvuvio, na kwa silika amwelekeze mnyama aikwepe hatari, na ndege, ni zaidi sana jinsi gani anavyopaswa kuwafanyia watoto Wake, waliozaliwa kwa Roho wa Mungu, wapate kuachana na mambo ambayo si ya kitauwa? Msiyakaribie, tokeni, egemeaneni. Loo, ninaipenda ile hadithi ya kale, ule wimbo, "Tunaegemea kwenye mkono wa milele." Ninaupenda huo. Mwaminini tu, urahisi wa tumaini, yaegemeze tu mabega yako kwa Yake, na kumwabudu Yeye kwa ibada zote ambazo unaweza kumimina, na kutembea pamoja Naye kila siku. Sasa, mtamwona.

107 Sasa, njia pekee mimi . . . Labda, usiku wa leo tuna Wamethodisti, Wabaptisti, na—na huku karibu sana na Meksiko labda tuna Wakatoliki wengi wa Kimeksiko, na kadhalika, wote wamechanganyika. Sasa, hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa. Mungu anawapenda watoto Wake wote. Wamechanganyikana katika madhehebu yote, wakimpenda Mungu, wakimtumaini Kristo kwa ajili ya wokovu wao.

Basi kama ningemwambia Mkatoliki, "Je, ungetaka kumwona Yesu?"

Vema, angesema, "Kanisa letu linamwakilisha Yeye."

Ningewaambia Wabaptisti, "Je, mnataka kumwona Yesu?"

"Loo, kanisa letu ndilo linalomwonyesha Yeye."

Wamethodisti, na Wapentekoste, na wengineo wangekuwa na wazo tofauti juu yake.

108 Nami nafikiri, usiku wa leo, kulileta kwenye—kwenye jambo rahisi, kwamba njia bora zaidi ya kujua Yeye ni nani, ni kurudi nyuma na kuona kile alichokuwa, kile alichokuwa jana, na kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, kile alichokuwa, hana budi kuwa ni kitu kile kile leo. Je, hilo lingetosha kwa makanisa yote? Ndipo unaweza—unaweza kujiridhisha mwenyewe, kama kanisa lako linalifundisha hivi au la. Tafuta kujua kile alichokuwa, na kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, kile alichokuwa, hana budi kuwa ni yeye yule leo.

109 Sasa, hebu turudi nyuma. Ninasoma kutoka katika Yohana Mtakatifu, mlango wa kwanza wa Yohana Mtakatifu, nasi

tutarudi nyuma tuone kile alichokuwa. Sasa, unaweza kulichukua na kuliendea kutoka mahali popote katika Maandiko. Tunaweza kufanya mkutano wa majuma mawili, na, juu ya kile tu alichokuwa, loo, majuma mawili, karne mbili, na kamwe tusipate kile alichokuwa. Lakini ili tu kupata ma—mambo machache muhimu ya kile alichokuwa, basi kama atakuwa ni yeye yule leo, papa hapa, kama alivyokuwa wakati huo, hilo linamfanya yeye yule. Hilo linapaswa kulitatua hilo swali. Mnaamini hilo? Hilo ni jema.

110 Sasa, tunaona ya kwamba Yeye alizaliwa kwa kuzaliwa na bikira; tulikuwa na hilo asubuhi ya leo. Na ndipo tunaona, mara baada ya Roho Mtakatifu kumjilia, aliongozwa mpaka nyikani, akajaribiwa na ibilisi siku arobaini, ndipo akatoka akihubiri Injili. Sasa, tunaona mwanzoni mwa huduma Yake alianza kuwaombea wagonjwa, wagonjwa wakiponywa.

111 Nasi tunaona ya kwamba kusanyiko Lake lilitoka kwa wa—watu maskini, wa—waliotengwa, wale ambao labda walitupwa nje, hawakuwa na elimu nyingi, kama yule mtu aliyempa funguo za Ufalme, Petro, hata asingeweza kuandika jina lake mwenyewe. Biblia ilisema alikuwa mtu asiye na elimu wala maarifa, bali kwa imani yake ilimpendeza Yesu kumpa funguo za Ufalme, kwa sababu alikuwa na ufunuo Wake.

"Watu husema Mimi, Mwana wa Adamu, kuwa ni nani?"

"Mmoja akasema, 'Wewe ni Eliya,' na mmoja akasema, 'Wewe ni yule nabii,' na 'Wewe ni *Nanii*.'"

Akasema, "Lakini ninyi mwasema ni nani?"

Akasema, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai."

112 Sasa, Katoliki inasema ya kwamba Yeye alilijenga Kanisa Lake juu ya Petro. Kama alifanya hivyo, alirudi nyuma mara moja. Basi, kama . . . Waprotestanti walisema alilijenga juu ya Yake Mwenyewe. Ninakanusha hilo, haikuwa juu ya Yake Mwenyewe, wala juu ya Petro, bali juu ya ufunuo.

113 "Nakwambia, wewe ni Simoni, wewe ni Petro. Mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia. Na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haiwezi kulishinda." Mnaona, ni—ni ufunuo wa Kristo. Kama anaweza kujifunua Mwenyewe, usiku wa leo, kwako kwamba Yeye yupo, basi uko katika Kanisa hilo kwa ufunuo.

114 Angalieni, hebu tuchukue huduma Yake ya mwanzoni, wa kwanza tunayetaka kuanza naye hapa alikuwa ni Andrea, mvuvi. Alimwona, na labda akarudi na kumwambia ndugu yake, Simoni, "Njoo uone Yule tuliyemwona. Tulimwona Masihi."

115 Sasa, walikuwa wakimtazamia Masihi. Walidhani Yohana alikuwa ndiye Masihi, watu wengi waliamini alikuwa ndiye. Lakini angalieni sasa, tutaona Yeye alikuwa ni nani.

116 Na wakati. . .Ninaweza kumwazia Petro akisema, “Sasa, hebu kidogo!” Bila shaka, jina lake lilikuwa Simoni wakati huo. Akasema, “Sasa, Andrea, labda umeingia wazimu mahali fulani, kwa namna fulani ya hamaki. Nitajua ajapo Masihi. Baba yangu mzee aliniambia, akasema, ‘Mwanangu,’ siku moja tulipokuwa tumeketi kando ya ziwa baada ya kuvua samaki, ninaweza kuona nywele zake zenye mvi wakati aliposema, ‘Simoni, mvulana wangu, baba yako daima ametamani kuona siku ambayo Masihi angetokea, lakini ninazeeka sasa na mimi, labda, sitaiona.

117 “‘Lakini Simoni, usisahau jambo hili, ya kwamba atakapokuja, kutakuwa na mambo mengi yatakayotukia. Huna budi kuwa, kumbuka Simoni, uwe wa Kimaandiko, Biblia inasema, masomo yetu yanatwambia, Musa, yule nabii, alisema, Masihi atakapokuja Yeye atakuwa ni Nabii, kwa maana imeandikwa katika Kitabu cha Torati, “Bwana Mungu wako atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi.”’” Je, hayo ni Maandiko?

118 “‘Basi kumbukeni, Yeye hatakuwa ninii, mtu wa madoido tu, bali atakuwa M—Mtu dhahiri, Nabii, Nabii mkuu, Mungu-Nabii, atakapokuja. Nanyi mmefunzwa vizuri katika hilo.’”

Kwa hiyo wakati Andrea alipokuja na kumwambia, “Njoo, umwone Yesu wa Nazareti, Yeye ndiye yule Nabii”:

119 Ninaweza kuwazia Simoni akisema, “Sasa, hebu kidogo, sijui kilichokupata, lakini, hakika, hamjasahau mafundisho ya Maandiko, lakini kwa ajili tu ya zamani za kale nitaambatana nanyi.”

120 Alipoenda Mbele za Bwana Yesu, Yesu alimtazama usoni na kusema, “Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona,” Petro alitambua upesi sana ya kwamba hapana shaka huyo ni Yeye, si kwamba tu Yeye alijua alikuwa ni nani, bali alijua baba yake alikuwa ni nani.

121 Kulikuwako na mmoja aliyesimama pale jina lake Filipo, yule tuliyesoma habari zake usiku wa leo, iliuchangamsha moyo wake hivi kwamba, ilimbidi kwenda kumwambia rafiki yake habari zake. Kuna kitu fulani kuhusu kumjua Yesu Kristo, ukiwahi kamwe kumpata Kristo halisi kweli, huwezi kutulia, huna budi kulisimulia mahali fulani.

122 Kwa hiyo tunamwona Filipo akizunguka kilima. Kama uliwahi kuwa huko Palestina, uone mahali Yesu alipokuwa akihubiria, karibu na mahali rafiki yake Nathanaeli alipoishi, ni kama maili kumi na tano. Hapana shaka alikimbia akauzunguka mlima huo. Hebu tuliigize tu kwa muda kidogo. Ninaweza kumwona akibisha mlangoni. Kuna watoto wadogo wagonjwa hapa, ninawataka walipate, imani yao ndogo, rahisi. Akabisha mlangoni, na labda Bibi Nathanaeli akaja mlangoni, akasema,

hakuwa na wakati wa kusalimiana sana, akasema, “Yuko wapi Nathanaeli?”

Kasema, “Loo, amerudi kwenye shamba la matunda, huko nyuma, akiomba, huko nyuma bustanini.”

123 Ndipo huyo akarudi bustanini. Nanyi mnajua mahali alipompata? Chini ya mti, akiomba. Ninaamini, Filipo akiwa ni Mkristo, hakumkatiza alipokuwa akiomba.

124 Baada ya kumaliza maombi yake na kusema, “Amina,” aliamka na kupangusa nguo zake, na papo hapo akatazama pande zote na kumwona rafiki yake Filipo, akasema, “Filipo, nina furaha kukutana nawe tena. Umekuja kunitembelea, ndugu yangu?”

125 Vema, kuna jambo fulani kulihusu, mtu anapomshika Mungu, naye Mungu anamshika huyo mtu, aliiendea hoja moja kwa moja, kasema, “Njoo, umwone Yule tuliyemwona, njoo umwone Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu.”

126 Na sasa, mwajua, Nathanaeli alikuwa mwaminio hodari wa kiothodoksi, kasema, “Sasa, ngoja kidogo, Filipo! Nimekujua kuwa mtu mzuri, mwaminifu, lakini hapo, je, laweza neno lolote jema kuja kutoka Nazareti?”

127 Sasa, nafikiri alimpa jibu zuri sana ambalo mtu yeyote angeweza kutoa, “Usikae nyumbani na kulikosoa, njoo, uone. Njoo ujionee mwenyewe, ulichunguze kwa Maandiko uone kama ni kweli.” Hilo ni wazo jema. “Njoo, ujionee mwenyewe. Usikosoe, njoo uone.”

128 Loo, ninawazia labda Nathanaeli alisema, “Sasa, ngoja, Yeye alipitia dhehebu gani?” Hilo lingekuwa toleo lake la 1961. Lakini hakusema, “Sasa, ngoja kidogo, tunajua Masihi akija, Yeye atamjia Kayafa—Kayafa, kuhani mkuu, yeye ndiye mwanadini mkuu kuliko wote nchini.” Ama, “Tunajua Yeye angekuja kwa askofu, ama mwangalizi mkuu, mtu kama huyo.”

129 Lakini Mungu huenda anakotaka, na afanyacho si kazi yetu. Yeye hufanya hivyo ili kujiridhisha Mwenyewe. Bila shaka. Hakumjia mtu yeyote, bali alikuja kwa maskini, na wavuvi, na katika hori, na—na wachungaji, na kadhalika.

130 Angalieni, basi walipokuwa wakienda zao, ninaweza kuwazia wakizungumza, wakiwa na ninii ndogo. . . kasema, “Unakumbuka. . . ? Sasa, Nathanaeli, wewe ni mwanachuoni hodari sana. Niambie, Nathanaeli, Masihi huyu atakuwa nini, tuliyeahidiwa? Tutamjuaje, kulingana na torati?”

Kasema, “Mbona, Yeye atakuwa ni Nabii, maana Musa alisema, ‘Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii mithili yangu.’ Atakuwa Mungu-Nabii.”

131 Mnajua Wayahudi daima wanaamini manabii wao, kwa kuwa Biblia ilisema, “Akiwepo mmoja miongoni mwenu aliye wa kiroho ama nabii, Mimi Bwana nitajifunua Mwenyewe

kwake. Na yale asemayo yakitimia, basi msikieni, kwa kuwa niko pamoja naye."

132 Hiyo ndiyo njia ya kuupambanua mkutano huu usiku wa leo. Kama Neno linasema hivyo, na Roho Mtakatifu ni wa kweli, atalidhihirisha, kama halidhihirishi, basi si Roho Mtakatifu. Hiyo ni . . . Lipambanue mwenyewe na kwa Neno.

133 Kisha akasema, "Unamkumbuka yule mzee mvuvi ambaye ulinunua samaki kutoka kwake wakati ule huko chini mtoni naye asingeweza kuandika jina lake kwenye risiti yako?"

"Naam."

"Unajua jina lake lilikuwa Simoni?"

"Naam."

134 "Ndugu yake alimleta mkutanoni jana kabla sijaondoka, na mara alipoenda Mbele za Yesu, alimwangalia na kusema, 'Jina lako ni Simoni.' Pia unamkumbuka baba yake?"

"Hakika."

"Basi Yeye alisema, 'Jina la baba yako ni Yona.'"

135 Huyo alikuwa ni Yesu jana, hivyo ndivyo Yesu alivyojitambulisha Mwenyewe kama Masihi. Kama hivyo ndivyo alivyofanya jana, itambidi kulifanya leo kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, Yeye atakuwa ni Mungu-Nabii.

Angalia kile alichofanya, alisema, "Haitanishangaza kama Yeye hakukwambia wewe ni nani utakapokuja mkutanoni."

"Aa, itanibidi kuliona."

136 Hatimaye wakawasili, labda aliingia kwenye mstari wa maombi ambapo Yesu akiwaombea wagonjwa, labda aliketi nje kwenye kusanyiko, sijui, lakini hata hivyo, wakati Yesu alipomkazia macho, Yeye alisema, "Tazama Mwisraeli kwelikweli, ambaye hamna hila ndani yake!"

Alimjuaje?

"Loo," unasema, "jinsi alivyovalia."

137 Loo, la, wote walivalia vile vile, watu wa mashariki, walivaa vilemba, angeweza kuwa Myunani, angeweza kuwa ni Mwarabu, walivaa vilemba na mavazi yaliyopwaya. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

138 Ilimshangaza *sana*, hata akasimama, na kusema, "Rabi," (*Rabi* maana yake ni "mwalimu.") "Rabi, ulinijua lini Wewe? Mbona, hujawahi kuniona maishani Mwako! Unajuaje kwamba mimi ni, nilikuwa Mwisraeli, na mtu mwaminifu na mwenye haki?"

139 Ninaweza kuona macho hayo yakimtazama tena, na kusema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona."

Loo, loo, loo, loo! Siku moja kabla, na maili kumi na tano kuzunguka milima. Ni macho ya jinsi gani!

140 Jamaa huyu alisema nini? Akasema, "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli." Hakika, alifundishwa, alijua la kuamini, alijua huyo alikuwa ni Nabii ambaye Musa alinena habari zake. "Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe mfalme wa Israeli."

Naye Yesu akasema, "Kwa sababu nimekwambia jambo hili, unaamini sasa?"

Akasema, "Naam."

Akasema, "Basi utaona makubwa kuliko haya, kwa kuwa utawaona Malaika wakishuka na kupanda."

141 Lakini kulikuwa na wengine waliosimama pale ambao hawakuamini hilo, wale wasomi mashuhuri wa siku hizo. Iliwabidi kujibu kusanyiko lao, kwa sababu kusanyiko lilikuwa liwaulize hilo swali. Kwa hiyo mnajua walichosema? Wasingeweza kujua jinsi Yeye alivyojua mambo hayo, kujua mawazo yao, na kadhalika, naye alikuwa ni Nabii Ambaye angeweza kuwaambia yaliyokuwako, na yaliyokuwa yanakuja, kuliona vizuri sana, maana Maandiko yalisema huyo angekuwa ndiye Masihi.

142 Na kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi jana, ishara iyo hiyo ndiyo ishara ya Masihi leo. Si kwa sababu mtu fulani alitembea mtaani akiwa na makovu mkononi mwake, damu na mafuta yakimtoka, ama chochote kile, akiwa amevaa joho, huyo angeweza kuwa ni mnafiki. Lakini ndugu, uhai ulio ndani ya mzabibu unaonyesha ni kitu gani.

143 Yesu alisema, "Mimi ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi." Kama tawi la kwanza lililotoka kwenye Mzabibu huo lilitoa kanisa la Kipentekoste, nao wakaandika Kitabu cha Matendo nyuma yake, kama Mzabibu uo huo ukitoa tawi lingine, watafanya jambo lile lile nyuma yake. Mzabibu huzaa zabibu.

144 Lakini mnajua, kama—kama watu wa magharibi hapa, niliona mchungwa hapa Arizona, ninaamini ulikuwa na aina nane ama tisa mbalimbali za jamii ya mchungwa juu yake, bali umepandikizwa. Na leo hii wengi sana wamepandikizwa Kanisani. Wao . . . Haliwezi kuzaa tunda. Ukiweka mchungwa na kuweka tawi la limau ndani yake, litazaa malimau, linaishi kwa uhai wa huo mti, bali linazaa tunda lake lenyewe, limau.

145 Na ndivyo ilivyo siku hizi, tuna makanisa yanayojiita makanisa ya Kikristo, bali yana alama za theolojia na za madhehebu. Lakini kama mzabibu huo wa Kipentekoste uliofanya kanisa la Kipentekoste kamwe ukizaa tawi lingine la Kipentekoste, litakuwa kama lilivyokuwa hapo mwanzo. Hiyo ni kweli kabisa. Kama Yesu Kristo akijitokeza Kanisani, atakuwa vile vile kama alivyokuwa huko nyuma. Hautazaa malimau wala

mabalungi, utazaa machungwa kama ni mchungwa na umezaa tawi lake. Halitakuwa ni mashirika, halitakuwa ni madhehebu, litakuwa ni Kristo, kwa usahihi.

146 Sasa angalieni, walisimama huku mikono yao ikiwa nyuma yao, walijua iliwabidi kujibu, kwa sababu Yeye hakuwanena mema, mbona, wao walisema, "Yeye anafanya hivi kwa nguvu za Beelzebuli."

147 Beelzebuli ni ibilisi, na mtu yeyote anajua kwamba kupiga ramli ni kwa ibilisi, mambo hayo yote ni ya ibilisi. Na kila kitu alicho nacho ibilisi ni kitu kilichopotoshwa kutoka kwenye kilicho halisi. Ibilisi hawezi kuumba, yeye si muumba; kuna Muumba mmoja tu, huyo ni Mungu.

148 Anaweza kupotosha kile ambacho kimeumbwa. Mwanamke mzuri anaweza kuwa ulimwenguni, mwadilifu na mwenye haki, ibilisi anaweza kumpotosha na kumfanya mwovu. Uongo ni nini? Ni ukweli ulioelezewa vibaya. Uovu ni nini? Ni haki iliyopotoshwa. Hilo ndilo . . . Kutokuamini ni nini? Ni imani iliyopotoshwa. Ibilisi hupotosha, ila hawezi kuumba, yeye si muumba; kuna Muumba mmoja, huyo ni Mungu. Angeweza kuumba chochote alichotaka kama angekuwa ni muumba; bali kuna Muumba mmoja tu, na huyo ni Mungu.

149 Sasa, tunaona hao jamaa pale wakisema ya kwamba Mtu huyu alikuwa akifanya hili kwa nguvu za ibilisi. Sikilizeni, sikilizeni kwa makini sasa, msikose hili. Yesu aliwageukia, na kusema, "Ninawasamehe hilo," kumwita Ibilisi, kumwita Ro—Roho wa Mungu aliyekuwa akifanya kazi hizo, ibilisi, kasema, "Ninawasamehe. Lakini siku moja Roho Mtakatifu anakuja kufanya jambo lile lile, nalo neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe katika ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ujao." Kwa hiyo mnaona mahali tunaposimama? Vema.

150 Tunaona huyo alikuwa ni Yesu jana. Loo, jinsi tungeweza kwenda jinsi ilivyokuwa huko chini katika mji wa Yeriko! Ninawazia maskini Zakayo alipanda juu ya mti, na kusema, "Sasa, nitamwangalia akipita. Lakini bila shaka, nilimsikia mke wangu akisema ya kwamba—ya kwamba Yeye angeweza kuyatambua mawazo ya nia, na kadhalika, bali sitaki Yeye anifanyie lolote la hayo, kwa hiyo nitaketi tu hapa juu ya mti na kuangalia."

151 Lakini wakati Yesu, akizunguka kwenye Barabara Kuu ya Haleluya na kuteremka kwenye Barabara ya Utukufu, alipopiga kona pale, basi hapa alisimama Zakayo juu ya mti, amejificha kabisa, labda jani, aliliinua tu, akichungulia nje, "Loo, ningetaka kumwona," akasema, "wakati akipita. Nilimsikia mke wangu akisema ya kwamba angeweza kunena mawazo ya moyoni, na angeweza kufanya mambo *haya*. Wananiambia Yeye ni Nabii, lakini nawaambieni Yeye hakika angekuwa ni

Nabii kujua mahali nilipokuwa. Lakini nitampumbaza sasa, niko nyuma ya vichaka hivi hapa, nimeketi kwenye tawi lililogawanyika."

152 Hapo ndipo watu wengi wanapoketi, mahali njia yako na njia ya Mungu zinapokutana, huna budi kupitia moja yazo.

153 Loo, mwangalieni ameketi pale juu, akichungulia juu ya jani hili, akiangalia chini. Yesu, akitembea moja kwa moja na kwa utulivu, akaja moja kwa moja chini ya mti, na kuangalia juu, kasema, "Zakayo, shuka uje, ninaenda pamoja nawe nyumbani leo." Loo, jamani! Huyo alikuwa ni Yesu jana. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele, ingekuwa ni Yesu leo.

154 Kumbukeni wakati alipoenda kwa. . .Hakufanya hivyo mwenyewe. Yohana Mtakatifu :19, tungeweza kuliendea hilo kwa ajili ya. . .Vema, tutaenda tu kwenye Yohana Mtakatifu 5:19. Yesu alisema, wakati alipopitia kwenye mlango uitwao Mzuri, na ama ma—mabirika, hasa, ya Bethesda. Nitalifikia hilo katika dakika chache, mlango wa Mzuri. Lakini Yeye—Yeye alipitia kwenye malango ya Bethesda, palipokuwa na kile kidimbwi. Na makutano makubwa ya viwete, vipofu, wasiojiweza, waliopooza wamelala pale, labda watu wa kila namna wanaoteseka, Biblia ilisema umati mkubwa. Naye akawapita, hakumgusa hata mmoja wao, hata hivyo amejaa huruma, amejaa upendo, akazunguka-zunguka mpaka akamwona mtu amelala kwenye godoro.

155 Ni wangapi wenu ninyi nyote mnajua godoro ni nini? Vema, mnatoka sehemu gani ya Kentucky? Nililelewa kwenye moja, kulala mlangoni katika hali ya joto.

156 Naye mtu huyu alikuwa amelala kwenye godoro, labda, hu—huenda alikuwa na ugonjwa wa tezi dume, ama huenda alikuwa na kifua kikuu, kilikuwa kimedumaa, alikuwa nacho miaka thelathini na minane. Lakini kumbukeni, Yesu alijua yote kukihusu, alijua mahali alipokuwa amelala, Naye akamjia, na kumwambia, "Wataka kuwa mzima?" Akiwapita hao wengine, "Wataka kuwa mzima?"

Akasema, "Sina mtu wa kunitia majini." Angeweza kutembea, kasema, "Wakati nikija," mtu mwingine anamshinda mbio, anatangulia kidimbwini.

Naye akasema, "Jitwike godoro lako, uende nyumbani kwako."

Ndipo Yesu akahojiwa juu yake. Kama akija kwenye mji huu na kufanya jambo lile lile usiku wa leo, angali angehojiwa.

157 Lakini alisema nini? Sikilizeni, Yohana Mtakatifu 5:19, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile." Yesu kamwe hakufanya mwujiza mmoja bila Baba kumwonyesha Yeye kwanza, au Yeye alisema kitu kibaya

hapo. “Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe.”

158 Hapana shaka walikuwa wakisema, “Kwa nini hukumponya Bw. Jones kule? Ameuza penseli mtaani kwa muda mrefu sana.”

159 “Huyu hapa maskini Dada Cashorn hapa, mbona, amekuwa na yabisi kavu kwa miaka mingi. Kwa nini hukumponya? Yeye ni mwanamke mzuri, yeye ni mshirika wa sinagogi langu.”

160 Akasema, “Ninafanya tu kama vile Baba anavyonionyesha Mimi. Baba anatenda kazi nami ninatenda kazi hata sasa.” Loo, huyo ni Yesu jana, huyo ni Yesu leo. Yesu yule yule anayetenda kazi kama Baba anavyomwonyesha; tunaliona.

161 Tunamwona mwanamke akipitia, naye akasema, “Laiti ningeweza kugusa upindo wa vazi Lake,” Yohana Mtakatifu, “kama ningeweza kugusa upindo wa vazi Lake ningepona,” naye akajipenyeza.

162 Sasa, Yeye asingeweza kuuhisi mguso wake kwa kuuhisi tu kimwili, kwa sababu vazi la Kipalestina linapwaya na lilikuwa na vazi la ndani la kuzuia mavumbi yasifikie viungo vyao. Ndipo walikuwa . . . Hiyo ndiyo sababu walitawadha miguu. Na upindo wa vazi Lake, nisingeweza kuhisi kama ungegusa koti langu, basi vipi kuhusu vazi hilo linalopwaya? Lakini Yeye aliihisi roho. Wanaume wote walikuwa wamemzunguka, lakini maskini mwanamke huyo alimgusa.

Naye akasimama, kwa maana alisema moyoni mwake, “Kama nikiweza tu kugusa upindo wa vazi Lake, nitapona.”

Ndipo Yesu akasimama na kusema, “Ni nani aliyenigusa?”

Ndipo Simoni Petro akasema, akamkemea, na kusema, “Kwa nini unasema jambo kama hilo?” Kasema, “Mbona, wote wanakugusa Wewe.”

163 Akasema, “Lakini naona kwamba nimekuwa dhaifu, nguvu zimenitoka.” Naye akaangalia kote kwenye kusanyiko mpaka akamwona maskini huyo mwanamke, naye akamwambia juu ya kutokwa kwake na damu, na kusema, “Imani yako imekuokoa.”

164 Huyo alikuwa ni Yesu jana. Na usiku wa leo, waulizeni makasisi, Biblia ilisema ya kwamba Yesu Kristo, usiku wa leo, ni Kuhani Mkuu aliye Utukufuni anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Kama ukimgusa Yesu usiku wa leo kama yule mwanamke alivyofanya, basi Yeye angetendaje? Angetenda vile vile alivyotenda wakati huo, kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, angegeuka na kusema, “Ulikuwa na *hiki-na-hiki*, lakini sasa imani yako imekuponya,” kama Yeye ni yule yule.

165 Sasa, kumbukeni, kuna ninii tu, tunapofunga, kuna matabaka matatu tu ya watu, ama mataifa matatu, kweli, ulimwenguni, hao ni watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi; hao ni wale wana watatu wa Nuhu. Tunaamini Biblia, ya kwamba jamii yote ya binadamu ilitokana na hao wana watatu, kama

tutaamini Neno, hao walikuwa ni Myahudi, Mmataifa, na Msamaria.

166 Sasa, kumbukeni, Wasamaria na Wayahudi, Msamaria alikuwa nusu Myahudi na Mmataifa, kwa hiyo walikuwa wakimtazamia Masihi. Na walio wa kweli kabisa moyoni, Yeye alijifunua Mwenyewe kwao, na huo ulikuwa ndio uamuzi Wake, kumbukeni, uamuzi Wake wa kujitambulisha kama Masihi kwa kuwaonyesha ishara hiyo.

167 Wale waliomwamini walikuwa na Uzima wa Milele, wale waliomkataa waliingia katika maangamizi ya milele. Sasa, tunamwona Yeye. . .Hivyo ndivyo alivyojitambulisha kwa Wayahudi. Tungeweza kwenda. . .Mwangalieni Bartimayo, kipofu na jinsi. . .Loo, ya—yale Maandiko tungeweza kuyarejea!

168 Sasa kumbukeni, Yeye pia alisema alihitaji kupitia Samaria, Yohana Mtakatifu 4. Alikuwa akienda Zake Yeriko, ilimbidi kuzunguka kilima kwenda Samaria. Na alipofika kule, Samaria, aliwatuma wanafunzi Wake mjini kununua chakula, ilikuwa mwendo wa adhuhuri.

169 Aliketi kisimani, mandhari ya kitu kama *hiki*. Na kulikuwako, ningesema, msichana mrembo aliyejitokeza. Tunamjua hapa Marekani kuwa ni kahaba. Alikuwa na makundi ya waume alioishi nao. Naye akatoka akaenda kuchota maji yake, labda ilikuwa ni kwa sababu alikuwa nje usiku kucha, kisha akalala mpaka adhuhuri. Kwa kawaida, wanawali huenda kisimani asubuhi na mapema.

170 Unapaswa kuwaangalia jinsi wanavyoyateka maji hayo kwa winchi, na kuweka mtungi wa galoni tano juu ya kichwa chao, na mmoja kwenye kila nyonga, na kutembea na kuzungumza kama wanawake wawezavyo, wala kamwe wasimwage hata tone lake. [Ndugu Branham anakohoa—Mh.] Lakini (Samahani.) sasa, lakini labda asingeweza kuambatana na watu wazuri, ilimbidi aje wakati hao wengine wote walikuwa wamechota maji yao.

171 Kwa hiyo tunamwona akija kisimani. Ndipo akaanza kuachilia maskini ninii—ninii yake, kuweka maskini hizo kulabu kwenye mipini ubavuni mwa—mwa jagi, kisha akaishusha apate kuchota maji, ndipo akasikia Sauti ikisema, "Mwanamke, nipe maji ninywe."

172 Ndipo akaangalia na kumwona Myahudi ameketi pale, kijana Mwanamume. Akaangalia, vema, alikuwa na umri wa miaka thelathini tu, bali Biblia ilisema alionekana wa hamsini, mnajua hilo, nadhani kazi Yake ilimfanyia hivyo. Vema, walisema katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 6, "Unasema ya kwamba umemwona Ibrahimu, nawe ni mtu asiyezidi umri wa miaka hamsini?"

Akasema, "Ibrahimu asijakuwako MIMI NIKO." MIMI NIKO alikuwa kwenye kichaka kilichowaka moto, mwajua.

Kwa hiyo, wakasema, "Wewe hujapata zaidi ya miaka hamsini."

173 Kwa hiyo, Yeye alikuwa ameketi ukutani na kumwomba mwanamke huyu maji anywe. Sasa, walikuwa na ubaguzi kule, kama walivyokuwa nao huko kusini. Akasema, "Si kawaida kwenu Wayahudi kumwomba Msamaria, mimi, mwanamke Msamaria, hilo si jambo la kawaida siku hizi." Sikilizeni hayo mazungumzo, msiyakose.

174 Yeye . . . Yeye akasema, "Kama ungalijua ni Nani unayesema naye," sijui, usiku wa leo, laiti kanisa kweli lingalijua Uwepo wa Bwana ulikuwa hapa, "laiti ungalijua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji unywe, nami ningekupa Maji ambayo huji hapa kuyachota."

Akasema, "Kisima ni kirefu, huna kitu cha kuchotea."

175 Basi mazungumzo . . . Alikuwa akijaribu kufanya nini? Kuwasiliana na roho yake. Baba alikuwa amemtuma huko juu, hakujua ni kwa nini, lakini mwanamke huyu akatokea, Yeye alikuwa akijaribu kuwasiliana na roho yake. Yeye akasema— Yeye akasema . . .

Mwanamke akasema, "Nyinyi mnasema tuabudie Yerusalemu, baba zetu waliabudu katika mlima huu, Wewe unasema huko Yerusalemu."

176 Yesu akasema, "Mungu ni Roho, nao wamwabuduo Yeye imewapasa kumwabudu katika Roho na kweli." Mazungumzo yakaendelea kwa dakika chache mpaka akapata shida yake ilikuwa ni nini. Sasa sikilizeni, itawafaa katika dakika chache. Mnaona? Alizungumza naye mpaka akapata shida yake, Naye akasema, "Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa."

Akasema, "Sina mume."

Angalieni, Yeye anawafanya hao Wasamaria sasa, Yeye tayari amekuwa kwa Wayahudi, kasema, "Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa."

Akasema, "Sina mume."

Akasema, "Umesema vema. Umekuwa na watano, kwa hiyo, yule unayeishi naye sasa siye mume wako, ulisema kweli."

177 Alifanya nini? Alijua mengi kumhusu Mungu kuliko nusu ya wahubiri wajuavyo, naye akiwa katika hali hiyo, zaidi ya walivyojua wakati huo, kwa vyovyote vile.

178 Akasema, "Bwana," hakumwita Beelzebuli, mpiga ramli, alisema, "Bwana, naona kwamba Wewe ni Nabii." Sasa sikilizeni, "Tunajua ya kwamba ajapo Masihi, ambaye anaitwa Kristo, Yeye atatuambia mambo haya," ishara ya Masihi, "sisi Wasamaria tunajua ya kwamba Masihi atafanya ishara hii, kwa hiyo huna budi kuwa ni nabii Wake."

Yesu akasema, "Mimi ninayesema nawe Ndiye." Loo, jamani!

179 Mnaona, alifundishwa kujua yale Masihi angefanya, si jinsi angevalia, bali kile angefanya, si aina ya mafundisho ambayo angekuwa nayo, bali . . .

180 Yeye alisema, “Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiniamini mimi.” Walijua Yeye angekuwa ni Mungu-Nabii.

181 Akasema, “Hapana shaka wewe ni nabii. Sasa, tunajua ajapo Masihi, ambaye anaitwa Kristo, Yeye atatwambia mambo haya yote,” mnaona, hiyo ndiyo ishara Yeye angefanya, “lakini ni Nani—u Nani Wewe?

Akasema, “Mimi Ndiye.”

182 Alifanya nini? Akaacha huo mtungi wa maji, akaingia mjini mbio, na kusema, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?” Nayo Biblia ilisema ya kwamba watu wa huo mji wakamwamini Yeye kwa sababu ya ushuhuda wa huyo mwanamke kwamba Yeye alimwambia shida zake. Kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara Yake jana, ni ishara Yake leo.

183 Sasa angalia, chunguza kote katika Maandiko na kamwe hutaona wakati mmoja alipofanya ishara hiyo mbele ya Mmataifa. Kwa nini? Mataifa, sisi Waanglo-Sakson, tulikuwa na marungu mgongoni mwetu na tulikuwa watu wa mapangoni, hatukuwa tukimtazamia Masihi yeyote, Masihi huja tu kwa wale wanaomtazamia.

184 Sasa katika kufunga, tamshi langu la mwisho, huenda nikasema hivi. Sininii . . . Ninaangalia ile saa huko nyuma na inanitia wasiwasi. Angalia, kuna mengi sana ya kusemwa, mengi sana ungeweza kuyaunganisha ndani.

185 Lakini sasa kumbukeni watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi, Wayahudi, Wasamaria, na Wamataifa. Sasa, Wayahudi na Wasamaria walikuwa wakimtazamia Masihi, Naye akajitambulisha Mwenyewe kwao kama Masihi kwa kuweza kuwaonyesha ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Nabii ambaye Musa alinena habari zake kwamba angekuja. Wote wanaoelewa, semeni, “Amina.” Vema.

186 Sasa, Mataifa wamekuwa na miaka elfu mbili, na sasa Mataifa wanafikia mwisho. Sasa, tulisema nini asubuhi ya leo? Kama Mungu akipata kufanya uamuzi na kufanya jambo lolote kwa njia moja, Yeye hana budi kulifanya wakati mwingine vivyo hivyo, la sivyo alikosea mara ya kwanza. Mnaelewa sasa?

187 Sasa, somo lingine moja dogo tu la Maandiko, samahani kwa muda kidogo tu, sina budi kuliweka hili hapa. Yesu alisema, katika Luka 16, ninaamini ndiyo, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Mliwahi kusoma hilo? Sasa, angalieni yaliyotukia Sodoma. Sasa, kwa makini sasa, tutaanzisha mstari wa maombi.

188 Daima kuna matabaka matatu ya watu: Ibrahimu aliwakilisha Kanisa lililoitwa litoke, Yeye aliitwa atoke, alijitenga na Sodoma; halafu kulikuwako na Wasodoma, wale waovu; na pia kulikuwako na Lutu na Mkristo wa—wa kawaida kule chini, mwaminio vuguvugu. Lakini alikuwa amejitenga na Ibrahimu, kwa sababu Ibrahimu alikuwa maskini sana, huko nje kwenye ardhi kame, na akachukua mahali penye utajiri.

189 Hivyo ndivyo makanisa makubwa, maarufu yamefanya siku hizi, matajiri, lakini kundi la kweli, Kanisa lililoitwa litoke . . . Sasa, kumbukeni, kuna matabaka matatu, mawili ya hayo yako huko chini Sodoma, Wasodoma; na pia mwa—mwaminio mkwamia mpakani, Lutu; halafu kulikuwa na Ibrahimu, Kundi lililoitwa litoke.

190 Siku moja alipokuwa ameketi chini ya mwaloni wake, kulitokea watu watatu, walikuwa wamevaa nguo kama wanadamu, wamejaa mavumbi, nayo ikasema walikuwa wageni, bali walikuwa ni zaidi ya wageni. Ibrahimu, akiwa mtu aliyejaa Mungu, akimwamini Mungu, mara tu alipowaona alijua kulikuwa na kitu cha kigeni juu yao. "Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu."

191 Na kwa hiyo, akatoka kuwalaki, na kusema, "Ingieni mkaketi chini ya mwaloni, nami nitawaletea maji kidogo, mkaoshe miguu yenu. Ndipo mle kipande cha mkate, kisha mwendelee na shughuli zenu."

Akaingia mbio hemani, akamwambia Sara, kasema, "Kanda unga kidogo, unga kidogo, pika keki chache mekoni."

Ndipo akatoka mbio na kumchukua ndama akamchinja, akampa mtumishi wake, na kusema, "Mtengenezeni."

192 Na walipomwandaa, wakamtoa nje, kisha wakaketi pale na kula, wanadamu, wakila kama wanadamu. Ndipo Mmoja akaendelea kuangalia chini kuelekea Sodoma. Hatimaye, wawili wao wakashuka kwenda Sodoma. Naye Huyu aliyebaki nyuma alimwambia Ibrahimu, kasema, "Sitakuficha nitakalofanya." Akasema, "Ni—nimesikia kuhusu Sodoma kuwa katika hali hiyo, nimeshuka kuja kuchunguza." Ibrahimu alijua huyo alikuwa ni Mungu.

Sasa, mhudumu mmoja aliniambia si muda mrefu uliopita nilipotoa tamshi hilo, akasema, "Unamaanisha kwamba mtu huyo alikuwa ni Mungu?"

Nikasema, "Ibrahimu alisema alikuwa hivyo, aliitwa Elohimu." Angalia kama si kweli, Elohimu.

Akasema, "Katika mwili wa nyama?"

193 Nikasema, "Kabisa. Hujui jinsi Mungu wetu alivyo mkuu." Nikasema, "Ninaweza kumwona akitembea kutoka Mbinguni, akinyosha mkono, tumeumbwa kwa elementi kumi na sita: petroli, potashi, na nurulimwengu, na petroli, alitwaa tu

konzi moja ya hizo, "*Whiu*!" Kasema, "Ingia hapa ndani, Gabrieli." Akanyosha mkono, akatwaa mwingine, akaingia, Malaika mwingine, akaingia ndani ya mmoja Mwenyewe, kisha akatoka moja kwa moja humo tena.

194 Nina furaha sana ninamjua, siku moja wakati mimi si kitu ila mavumbi, Yeye ataniita, nami nitamjibu, anaweza kukuita, utaitika. Yeye ni Elohimu, Yule Ajitoshelezaye kwa yote. Bila shaka.

195 Sasa angalieni, angalieni ishara aliyomfanyia mwaminio, Kanisa lililoitwa litoke. Sasa, kulikuwako na Billy Graham wa kisasa, na hao wengine, walishuka na kuwahubiria huko Sodoma, hawakufanya miujiza yoyote, ila tu waliwapofusha. Vema, Injili humpofusha asiyeamini kwa vyovyote vile. Kwa hiyo, hawakufanya miujiza yoyote, bali walimwita Lutu kutoka mle, yeye, na mke wake, na watoto kutoka Sodoma.

196 Lakini mwangalieni Yule aliyekuja kwa Kanisa Teule, lile lililo katika uchache, karibu, Yeye alikuwa ameuelekeza mgongo Wake kwenye hema. Wanawake katika siku hizo, si kama walivyo sasa, inawabidi kukimbia na kuchukua mahali pa waume zao, na kufanya maongezi yote, walikaa huko nyuma mahali pao hemani. Kwa hiyo basi Yeye alikuwa . . . Hawakuwa wajasiri jinsi walivyo, loo, jamani. Vema, mimi . . . Hilo lote ni jukumu lenu, ndugu, nyosheni hilo.

197 Lakini kwa vyovyote vile, angalieni, Mtu huyu aliketi huku mgongo Wake umeelekezwa kwenye hema, Naye akasema, "Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?" Alijuaje alikuwa ameoa? Alijuaje jina la mkewe lilikuwa Sara?

Sasa angalieni, Biblia ilisema, Ibrahimu alisema, "Yuko hemani nyuma Yako."

198 Naye akasema, "Ibrahimu, *Mimi*," hicho kiwakilishi nafsi tena, "Nitakuzuru kulingana na ahadi niliyokupa." Sara alikuwa na umri wa miaka tisini wakati huo, "Nitakuzuru kulingana na ahadi niliyokupa ya kwamba utampata mtoto huyo."

Naye Sara, akiwa hemani, akacheka moyoni mwake, kasema, "*Hmmph*!"

199 Ndipo yule Malaika huku mgongo Wake umegeuzwa akasema, "Kwa nini Sara akacheka?" Hiyo ilikuwa ni nini? Alijua jina lake lilikuwa Sara, akampa ahadi, na alijua aliicheka, nafsini mwake, hemani.

200 Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Mataifa walikuwa na miaka elfu mbili ya theolojia, sawasawa na Wasamaria na hao wengine. Sasa, ilikuwa ni nini? Malaika, Mungu, kuwa akifanya kazi katika mwili wa mwanadamu.

Hivyo ndivyo ilivyokuwa, ilikuwa ni Mungu katika umbo la mwanadamu.

201 Sasa, Kristo, alipokufa, alilitakasa Kanisa, ili kwamba Yeye Mwenyewe aweze kurudi na kuishi katika Kanisa hili, na kufanya mambo aliyofanya, "ninyi nanyi mtayafanya." Hiyo ni kweli? [Ndugu Branham anasafisha koo lake—Mh.] (Samahani.) Sasa, kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, atafanya kama alivyofanya jana, na atafanya hivyo leo, na atafanya milele. Hiyo ni kweli?

202 Sasa, "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Yuko wapi siku hizi? Yuko katika Kanisa Lake. Kanisa Lake ni nani? Walioitwa watoke. Atafanya ishara ya namna gani? Kama alivyoahidi. Atalishughulikiaje? Vile vile alivyofanya wakati alipomjia Ibrahimu, vile vile alivyofanya alipowajia Wayahudi, vile vile alivyofanya wakati alipowajia Wasamaria, na kuahidi hilo mwishoni mwa wakati wa Mataifa.

203 Sasa, kama tunaweza kumwona akija jukwaani . . . Haidhuru angenitia mafuta kiasi gani, hana budi kukutia mafuta, pia. Wakati alipokuja kwenye mji Wake Mwenyewe, asingeweza kufanya kazi nyingi kuu kwa sababu ya kutokuamini kwao. Kwa hiyo hana budi kuwatia mafuta, Naye hana budi kunitia mafuta. Na hilo linawafanya walimwengu kuona ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule, kwa sababu Yeye anafanya kazi katika Kanisa Lake katika mwili wa kibinadamu ambao ameutakasa kwa Damu Yake Mwenyewe, kwa kusudi la kujidhihirisha Mwenyewe, akijifanya Mwenyewe yeye yule jana, leo, na hata milele.

204 "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena." Sasa, *ulimwengu* ulioandikwa hapo ni neno la Kiyunani *kosmos*, ambalo linamaanisha "utaratibu wa ulimwengu," Mnaona? "Ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona," *ninyi*, huyo ni mwaminio, Kanisa, "kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.

205 Mnaamini hilo? Kwa ahadi hizi chache ambazo nimewaambia usiku wa leo . . . Si kwa sababu Yeye alivalia tofauti, si kwa sababu Yeye alikuwa wa ukoo wowote, si kwa sababu Yeye alikuwa mfuasi wa dhehebu fulani, hakukuwako na kitu kama hicho katika siku hizo, ambacho hakikumfanya Yesu, ambacho hakikumfanya Mungu, bali kazi alizofanya zinathibitisha ya kwamba agizo Lake alilosema alitumiwa lilikuwa ni kweli. Hiyo ni kweli? Vema, ikiwa Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, naye aliahidi kazi zile zile alizofanya Kanisa lingefanya, hivi hamwamini hilo? Kama likifanya hivyo, basi maneno Yake ni kweli.

206 Basi kama aliwafanyia Wasamaria, na Wayahudi, na kuliahidia Mataifa katika siku ya mwisho kabla ya Kuja

kwa Mwana wa Adamu...Loo, tunaishi katika siku gani, ndugu? Tuko hapa. Tuko katika wakati wa mwisho, ndugu, dada. Linaweza kutukia karibu wakati wowote. Kumbukeni, walipolikataa, mnajua kilichotukia, Sodoma iliteketezwa, Wayahudi wakaangamizwa, na sasa tuko kwenye wakati wa Mataifa wa miaka elfu mbili.

207 Sasa sikilizeni, nabii alisema, "Kutakuwako na siku ambayo itakuwa na utusitusi, haiwezi kuitwa usiku wala mchana, lakini wakati wa jioni itakuwa Nuru." Hiyo ni kweli? Sasa, jua lile lile linalochomoza mashariki, hutua magharibi. Yule M-w-a-n-a aliyekuja mashariki kwa watu wa mashariki, na kuwamwagia Roho huko mashariki . . .

208 Tumekuwa na miaka elfu mbili ya madhehebu ya kanisa, siku yenye huzuni tu, vya kutosha kuona jinsi ya kujiunga na kanisa na kuishi maisha mazuri, lakini ni wakati wa machweo ya jua, Mwana yeye yule, akiwa na kitu kile kile alichokuwa nacho mashariki, anakiangaza duniani tena magharibi. Nasi tuko kwenye Pwani ya Magharibi, kama tukienda mbali zaidi, ustaarabu umesafiri pamoja na jua, tungerudi mashariki tena. Kwa hiyo tuko katika wakati wa jioni pamoja na Nuru ya jioni, pamoja na Roho Mtakatifu yeye yule aliyekuwa juu Yake yuko ndani ya Kanisa akifanya mambo yale yale. Yesu Kristo yeye yule jana, leo na hata milele.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

209 Mungu mwenye rehema, Neno moja kutoka Kwako litakuwa zaidi ya mtu yeyote angeweza kusema maishani. Tunasoma ya kwamba ni kweli, Ee Mungu, bali watu wanasema sasa, "Hebu tuone kama linafanya kazi." Hakika, Bwana, halina budi kutenda kazi, halina budi kulenga shabaha, halina budi kuwa hivyo, Wewe uliahidi hilo. Ninaomba ya kwamba utajidhihirisha Mwenyewe usiku wa leo, Bwana. Watu hawa wanakupenda, nao ni wagonjwa. Mtu huyu aliyeketi hapa, amemshika mtoto huyu mdogo mwenye kichwa kilichojawa maji, maskini baba huyu aliyeketi hapo akikohoa, mama huyu aliyeketi kwenye kiti cha magurudumu; mmoja kule akiwa na fimbo, nyeupe, mkononi, Ee Mungu, wanalia:

Usinipite, Ee Mwokozi mpole,
Sikia kilio changu kinyenyekevu;
Unapozuru wengine,
Usinipite.

Kwako Wewe uliye Kijito cha faraja yangu yote,
Zaidi ya maisha kwangu,
Ni nani niliye naye duniani mbali na Wewe?
Au ni nani Mbinguni ila Wewe?

210 Na ijulikane usiku huu, Bwana, nimenena habari Zako. Sasa nena kwamba nimesema kweli, Baba, hiyo itathibitisha

hayo maneno na watu hawa wataamini, nao wataponywa na kwenda nyumbani wenye furaha. Pia jalia kwamba kutakuwako na uamsho utakaotokea hapa katika jiji hili, yapata maelfu ya watu watavutwa kwa Kristo, na kila kanisa litajaa watu, makanisa mapya yatajengwa. Na jalia iwe ni mfano kwa watu wapate kuja kutoka mashariki na magharibi kuuona utukufu wa Mungu. Tujalie, Bwana.

211 Tunayakabidhi yote mikononi Mwako sasa. Nimemaliza, hakuna mengine ninayoweza kusema, ni juu Yako kunena sasa, Baba, kwa sababu watu wanaona ni ahadi. Dakika chache tu hapa kutoa hotuba kidogo, ninatumaini ya kwamba Roho Mtakatifu ataliingiza Neno moja kwa moja ndani kabisa ya moyo wao, hata hawatashindwa kulipata. Ninaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

212 [Ndugu Branham anakohoa—Mh.] Samahani kwa kikohozi changu. Ninahubiri wakati wote, nami nina koo la mhubiri tu, na hivi majuzi nililowa maji sana, na kwa namna fulani nimekuwa na kikohozi kikavu tangu nilipokuwa huko juu—huko Beaumont, Texas.

213 Kwa hiyo sasa, na—nawatakeni mkumbuke. Sasa, kama tungeweza kumwona usiku wa leo akija na kufanya kama tu alivyofanya wakati huo, je, tungekuwa kama wale walioenda nyumbani kutoka Emau? Walitembea siku nzima pamoja Naye wala hawakujua. Usiku huo alitenda kana kwamba angepita. Huenda akatenda vivyo hivyo kwako usiku wa leo, kana kwamba atakupita. Huenda usiwe na kadi ya maombi, huenda hata usiwe mstarini, bali Yeye hatakupita. Mwalike tu, useme, "Jalia nikuguse, Bwana." Angalia yale afanyayo.

214 Loo, hiyo si ni changamoto? Wazieni hilo. Ni changamoto zaidi kuliko kumwendea mwanamke huyu kwenye kiti cha magurudumu, na kusema, "Simama utembee." Bila shaka. Kwa kweli angeweza kufanya hivyo kupitia nguvu za kiakili, kweli, kiakili, angeweza kufanya hivyo kwa misingi ya Sayansi ya Kikristo, imefanyika. Lakini unapomwona Kristo akija ndani ya watu na kufanya madhihirisho yale yale ya ishara ya Mbinguni, iliyotolewa tena katika kulitimiza Neno, ni mwujiza wa jinsi gani, ni nguvu za jinsi gani!

215 Na kuwazia, mimi hapa katika jengo hili usiku wa leo, hakuna mtu hapa ninayemjua, ambaye ninaweza kumwangalia na kuona, hakuna ila mvulana wangu wa kanda aliyeketi papa *hapa*, Ndugu Goad; yeye ndiye mtu pekee ninayemjua. Mungu anamjua kila mmoja wenu. Sasa, mimi si Yeye, Yeye yupo hapa, hata hivyo.

216 Na sasa, hatuwezi kuziita kadi hizo zote za maombi kwa wakati mmoja. Nami ningetaka tu waje wachache tu kwa wakati mmoja, wakati wakiitwa, ama kungoja kidogo. Nina hakika alisema alisambaza kadi. Billy yuko wapi? Wapi? Loo, samahani.

Naam. Za A? Moja hadi mia moja? Vema. Hebu tuanzie kwenye moja, namba moja basi. Ni nani aliye na kadi ya maombi namba moja A? Nitawaita, ili tuweze kuwabeba wale walio kwenye viti vya magurudumu na kuwachukua. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

217 . . . Biblia na hicho kingine, nilisema, "Vyote viwili haviwezi kuwa sahihi, Kimoja ni cha kweli na hicho kingine ni cha uongo. Acheni Mungu wa Biblia anene."

218 Afrika Kusini, vivyo hivyo, mbele ya yapata watu mia mbili na hamsini elfu, loo, Yeye angali ni Mungu, wakati wale wachawi, walipotahayarishwa tu, wakisimama pale, adui akifukuzwa. Kesho yake asubuhi yapata malori saba ama manane makubwa ya mikongojo tu, na viti vya magurudumu, na mbao nene walizokuwa wamebebewa, yalikuwa yakishuka kwenda barabarani, wakati Sidney Smith, Meya wa Durban, aliponipigia simu, akasema, "Ndugu Branham, angalia nje ya dirisha lako, kuelekea ufukoni mwa bahari."

219 Wakaja mamia ya watu, siku iliyotangulia walikuwa kwenye mikongojo na viti vya magurudumu pamoja na magari saba makubwa mno ya Kiafrika, marefu kama hizo nguzo mbili pamoja, vimelundikwa hata pomoni, yamejaa hivyo, wakija huku wameinua mikono yao juu, wamekuwa wakipigana katika makabila, wakitembea kesho yake wakiimba, "Mambo yote yanawezekana; amini tu."

220 Ishirini na tano elfu waliponywa kwa wakati mmoja. Kwa nini? Hawakuwa wameshindiliwa kabisa na kila kitu, walikuwa bikira, waliisikia Biblia, wakaiamini, wakaikubali, ndipo ikatukia.

221 Sasa iweni na kicho kabisa, kaeni vitini mwenu, iweni kimya. Simaanishi kusema hamwezi kumsifu Mungu, bali nyamazeni tu na msikilize. Sasa, sasa katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, Ninachukua kila roho humu ndani chini ya mamlaka yangu kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Sasa iweni waangalifu baada ya jambo hilo.

222 Sasa, nakisia ya kwamba katika mstari huu wa maombi hapa, kila mmoja wenu ni mgeni kwangu. Hiyo ni kweli? Inua mkono wako. Kama hatufahamiani, inua mkono wako. Sikujui wewe.

223 Sasa, kama ningeweza kukuponya na nisingefanya hivyo, ningekuwa mnafiki. Ila siwezi kufanya yale Mungu tayari amefanya. Ninaweza tu . . . Vipi kama angalikuwa amesimama hapa usiku wa leo amevaa suti hii aliyonipa? Wewe useme, "Bwana, utaniponya?"

Unajua kile Yeye angesema? "Mtoto wangu, tayari nimefanya hivyo, siwezi kulifanya mara mbili, nilifanya tu mara moja. Ni, huna budi kuamini."

224 Lakini basi huenda akakuonyesha—akakuonyesha jambo fulani kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi. Sasa, si kwa alama za misumari, maana mtu yeyote angeweza kuwa na alama za misumari mikononi mwake. Lakini angefanya ishara ile ile aliyofanya mara ya kwanza, kama alivyoahidi angefanya. Kamwe hatakiuka ahadi Zake, yale aliyoahidi atafanya.

225 Sasa, huyu hapa mwanamke, hatufahamiani. Vema. Umesoma vitabu vyangu. Alisema alikuwa amesoma vitabu vyangu, naye alidhani karibu alinijua kwa kusoma vitabu vyangu. Vema. Basi, dada yangu, nina mama nyumbani, usiku wa leo, ananiombea. Sikushuka kuja hapa kuwa mdanganyifu, nilikuja hapa kuwa ndugu. Sikuja kupachukua mahali pa daktari, nilikuja kuwasaidia wagonjwa wake, mnaona, wapate kupona. Sikuja nikiwakilisha kanisa lolote, Bwana Yesu Kristo tu.

226 Sasa, hii ndiyo mara ya kwanza, nijuavyo mimi, tumewahi kukutana. Basi kama ningekuja, ungeninii, labda, kama uko kwenye mstari wa maombi, ungekuwa mgonjwa, na kama ningesema, nikimbie, nikuwekee mikono yangu, niseme, "Pokea uponyaji wako katika Jina la Bwana Yesu. Nenda, amini," ungekuwa na haki ya kufanya hivyo. Hiyo ni kweli, hiyo ni kweli.

227 Lakini sasa, vipi kama Yeye angekuja hapa na kukwambia jambo fulani ambalo umefanya, ama kama alivyomfanyia yule mwanamke kisimani, akazungumza naye na kumfunulia kile—kile shida yake ilichokuwa? Basi ungejua ya kwamba haikuwa ni mimi, sivyo? Maana sikujui. Sijawahi . . . Hii hapa mikono yangu, ni—ninamwinulia Mungu mikono yangu juu ya Biblia Yake, sijawahi kumwona maishani mwangu, sijui lolote kumhusu. Na hiyo ni kweli, sijui mtu hata mmoja kwenye mstari huo wa maombi, ama popote pale kama ninavyoweza kuona, ila wale niliowaita kwa jina.

228 Lakini sasa, Kristo anadumu yeye yule, sivyo? Sasa, kama Yeye ataninii . . . Kama mwanamke huyu . . . Na awe ndiye mwamuzi, kama nyote mnamjua hapa kanisani ama popote anapotoka. Kama—kama yeye . . . Kama Yeye anaweza kumwambia kile amekuwa, na ana shida gani, ama kilichomleta hapa, huenda ikawa ni mambo ya nyumbani, ya kifedha, si—sijui. Lakini kama anaweza kufunua hilo, je, hilo litamfanya yeye yule jana, leo, na hata milele? Ni wangapi watakaoamini hilo? Sasa, inua mkono wako, useme, "Nampenda, na ninamwamini." Asanteni, karibu asilimia mia moja. Mnaona?

229 Sasa, kama huamini hilo, afadhali unyamaze, maana unajua kinachotukia, mara nyingi mateso hutoka kwa mmoja hadi mwingine, hayana budi kupata mahali. Mnakumbuka katika Biblia? Mnaona? Yatatoka kwa mmoja hadi kwa mwingine. Loo, nimeona mengi sana yakifanyika namna hiyo. Kwa hiyo kama tu

ndugu, nasema kama huamini hilo, afadhali uketi tu kwa kicho, na kuinamisha kichwa chako chini mpaka itakapokwisha.

230 Sasa, maneno ambayo nimenena juu ya Yesu Kristo sasa hayana budi kudhihirishwa, ama nimesema uongo, au Biblia Yake imesema jambo ambalo si kweli. Sasa, kama mtu yeyote haamini hilo, anataka kupachukua mahali pangu, umekaribishwa kupanda hapa juu na kupachukua, mnaona.

231 Lakini maadamu Mungu alifanya ahadi, Yeye hutimiza ahadi Yake. Na wakati Malaika wa Bwana alipokutana nami huko juu miaka kumi na minne iliyopita, na kuniambia mambo haya niliyozaliwa kufanya, na kulijua maishani mwangu mwote, huku ndugu wa Kibaptisti wakijaribu kuniambia ilikuwa ni ibilisi na kadhalika, ndipo nikaja kugundua, ilikuwa ni Mungu mwenyewe wa Mbinguni akijaribu kunifikia. Nimeliamini tangu wakati huo. Imeushtusha ulimwengu. Nimeona mamilioni hasa wakimjia Kristo kote ulimwenguni.

232 Sasa hii hapa Tucson kwa mara ya kwanza. Hii hapa katika Biblia. Hii hapa ahadi; lakini je, itafanya kazi? Itafanya kazi atakapoitumikisha Yeye, na ni hayo tu.

233 Sasa, kama Bwana akinifunulia shida ya mwanamke huyu, ni wangapi watakaomkubali Yeye kama Mponyaji wako? Na hapa tukiwa sote wawili tumeinua mikono yetu, hatujawahi kukutana hapo kabla maishani. Alisema alikuwa amesoma vitabu vyangu, kwa hiyo ana fununu ya kile kingetukia kama Yeye angefanya hivyo. Sasa, kama atafanya hivyo au la, kumbukeni sijui mimi. Asipofanya hivyo, basi nitashuka tu kwenye mstari wa maombi, nikiwaombea wagonjwa, na kuuacha uende hivyo, hilo tu ndilo ningaliweza kufanya. Lakini Yeye kamwe hajanipungukia, siamini atanipungukia usiku wa leo.

234 Ninataka kuzungumza nawe kwa dakika moja tu, kwa kuwa wewe ndiwe mtu wa kwanza, kama vile Bwana wetu alivyomfanyia yule mwanamke kisimani, Yeye alikuwa akijaribu kuwasiliana na roho yake. Nzuri sana, ingekuwa ni mwanamke, wa kwanza kwenye mstari wa maombi, ndiyo kwanza nimalize hayo katika Yohana Mtakatifu 4. Sasa, ninaweza tu kumwona Yeye ameketi pale, na kumwona yule mwanamke akitoka kuja kuchota maji, Naye anaanza kumhoji.

235 Ninaamini, sasa, ita—itawabidi tu kuamini neno langu kwa jambo hilo, ninaamini alikuwa akijaribu kuwasiliana na roho yake. Baba alikuwa amemtuma huko juu, alikuwa na haja ya kupitia, Naye alisema hakufanya lolote mpaka Baba alipomwonyesha, kwa hiyo ilimbidi Baba kumwonyesha Yeye kwanza. Baada ya kitambo kidogo akapata kujua shida yake ilikuwa wapi, Naye akamwambia shida yake ilikuwa ni nini.

Naye akasema, "Vema, hiyo ndiyo ishara ya Masihi! Ninajua atakapokuja, Yeye atatuambia mambo yote, kwa hiyo hapana shaka Wewe ni nabii."

Akasema, "Mimi Ndiye." Basi akaenda akaupasha habari huo mji.

236 Huo ungekuwa ndio mtazamo wako kwake? Ukijua ya kwamba mimi nikiwa ndugu yako, wala sikujui, sijawahi kukuona maishani mwangu, nasi tumezaliwa labda umbali wa maili kadhaa, na tumeachana kwa miaka kadhaa, na hii hapa mara yetu ya kwanza kukutana, na kama atanifunulia shida yako ni nini, utamkubali kama Masihi? U—utamkubali? Unamkubali.

237 Huyu mwanamke ametiwa uvuli wa mauti. Kuna kivuli cheusi kinachoning'inia juu yake, naye anaugua kansa. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sasa, unaamini hilo?

238 Sasa, ninahisi hilo likinijia tena, "Yeye alibahatisha hilo." Usiwazie hivyo. Huwezi kujificha sasa, Yeye yupo hapa. Mnaona? Tayari limetiwa mafuta sasa. Kamwe sikubahatisha hilo. Vema, ngojeni kidogo, hebu tukomeshe hilo sasa.

239 Wewe ni mtu mzuri. Sijui alichokwambia, jambo pekee alilokwambia, sina budi kulipata kwenye kanda hii hapa na kuona yale aliyosema. Ni kama tu kurudi chini kupitia mkondo wa uhai mahali fulani na kulipata. Sasa ninaiona ikija tena, naam, ni kivuli, ni giza, ni kansa. Sasa, kama nitakwambia mahali hiyo kansa ilipo, utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Iko kwenye matiti yote mawili. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

240 Jambo lingine kwa hilo, daktari wako alikwambia inaingia kwenye uti wa mgongo, pia. Lakini hiyo ni kweli, ikipenya kwenye uti wa mgongo; ni majaliwa. Kama Bwana Yesu ataniambia wewe ni nani, je, hilo litamfanya Yeye Mungu yeye yule Ambaye angeweza kusema . . .? Hiyo ni kweli? Bibi Hall, hiyo ni kweli. Hutoki hapa. Umetoka nchi yenye baridi, baridi sana, na imejaa milima, ni Colorado. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Je, unamwamini kwa moyo wako wote? Rudi, na uponywe katika Jina la Yesu Kristo basi. Na baraka Zake na rehema zikae juu yako, na kukupa ninii . . .? . . . ya Roho Mtakatifu. Mnamwamini Yeye? Mungu awabariki.

Mnaamini? Aminini, aminini sasa. Sasa, mmeshawishika ya kwamba Yeye ni Masihi yule yule? Sasa, si mimi, ni Yeye.

241 Sasa, msi—msisogee huku na huku, jamani. Mnaona, kila mmoja wenu ni roho, na kila wakati mnaposogea, inanisumbua sana. Mnaona? Kaeni kimya, kaeni kimya kabisa, nyamazeni. Angalieni huku. Kamwe msisogee, mnaona, kila mmoja wenu ni roho na upako huo unapokuja, ni—ni kama tu kijito, mnaona. Nami ninawasiliana nanyi, nanyi mnawasiliana na Mungu. Mnapowasiliana na Mungu, Yeye hunena tu kwa njia Yake . . .

242 Maikrofoni hii ni—ni bubu, haina budi kuwa na kitu cha kuizungumzia, vivyo hivyo na mimi, ni bubu tu juu ya mambo

haya, haina budi kuwa na kitu cha kuzungumzia. Kwa hiyo kila mmoja unaposogea, ama unapoenda huku na huku, ama kufanya jambo fulani . . . Mnaona? Yesu alimpeleka mtu nje ya mji wakati mmoja kupata . . . Mnaona? Iweni tu na kicho kabisa, angalieni. Sasa, ukitaka kumsifu Mungu, hilo ni sawa, lakini usiamke na kutembea-tembea, unajua, na mambo kama hayo, hu—hutatiza. Yeye, Roho, Roho Mtakatifu ni mwoga sana, mwoga sana. Bila shaka, hamkujua, labda, mpaka sasa, lakini iweni na kicho kabisa.

243 Sasa, mtu mwingine yuko wapi? U hali gani? Sijarukwa na akili, bali ni upako. Wewe ni kijana hodari sana. Je, unaniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu? Hivyo ndivyo Malaika alivyosema, "Kama unaweza kuwafanya watu wakuamini, kisha uwe mwaminifu unapoomba."

244 Sasa, wewe ni msichana tu, wala sijawahi kukuona maishani mwa—mwangu, nadhani hatufaha- . . . Nadhani wewe ni Mhispania. Wewe . . . Lakini sikujui, nawe hunijui, nasi tumeketi tena usiku wa leo kama tu ilivyokuwa katika Yohana Mtakatifu 4 tena, mwanamke. Sijui lolote kukuhusu. Sisi ni mataifa mawili ya watu. Wewe ni msichana tu, nami ni mwa—mwanaume mwenye umri wa makamu, bali tunakutana kwa mara ya kwanza. Lakini ikiwa Mungu wa Mbinguni, aliyemtuma Mwanawe, Kristo Yesu, na kumfufua katika wafu, na kumtuma tena Roho Mtakatifu katika Jina Lake, na kuahidi, "Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya . . . " Unaamini sasa ya kwamba unasimama katika Uwepo Wake, si wangu?

245 Una hisia ya kipekee, kwa sababu Nuru hiyo inatulia moja kwa moja juu ya msichana huyo. Unaona? Ninakutaka useme jambo hili kwa wasikilizaji kama hili ni kweli, hisia tamu sana nyenyekevu inakuzunguka. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako ili kusanyiko liweze kuona. Ninaiangalia moja kwa moja ile Nuru iliyo karibu na huyo msichana.

246 Huko hapa kwa ajili yako mwenyewe, si ugonjwa wako, uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine, mtu huyo yuafa. Mtu huyo ana kansa, nayo kansa hiyo iko kwenye tezi, nami ninaamini daktari alitangaza tu ni lukemia, anauita, katika mkondo wa damu. Hiyo ni kweli. Mtu huyo hayupo hapa, kutoka Mexico, shemeji yako. Hiyo ni kweli, sivyo? Amini sasa, amini ya kwamba ataponywa. Kulingana na imani yako, ndivyo itakavyokuwa. Nenda, na amani ya Mungu ikae juu yako, mtoto wangu.

Baba Mungu, bariki haja yake naomba, katika Jina la Yesu. Amina.

Amini sasa kwa moyo wako wote, amini tu. Unatilia shaka chochote? Usiwe na shaka. Amini kwa moyo wako wote.

247 Msipige picha sasa hivi, sasa, mnaona, ni—ni Nuru, sina budi kuifuata hiyo Nuru, mnaona.

248 Vema, huyu hapa msichana amesimama hapa. Simjui, sijawahi kumwona maishani mwangu. Hatufahamiani . . . Yeye hazungumzi Kiingereza. Hiyo ni kweli. Mimi . . . Unaweza, mtu fulani hapa anaweza kufasiri, unaweza—unaweza kuja hapa? Asante, simama tu hapa. Ninii tu . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . yale ninayosema sasa, maana haina budi kuingia chini ya upako, mnaona. Sasa, huyu mama hazungumzi Kiingereza, kwa hiyo msichana huyu atanifasiria.

249 Sasa, huyu hapa mwanamke nisiyemjua, hata sizungumzi lugha yake. Mimi ni mgeni kwako. Kama Mungu atanifunulia kilichokuleta hapa, utamwamini? Utaniamini kama mtumishi Wake? Basi mimi ni mtumishi Wake, na basi Yeye atanifunulia kilichokuleta hapa, ndipo ujue itabidi iwe ni Yeye, wala si mimi. Huko hapa kwa ajili yako mwenyewe, uko hapa kwa ajili ya mtoto wako mchanga. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

250 Kama Mungu atanifunulia shida ya mtoto wako mchanga, utakubali uponyaji wake? Mtoto mchanga anasumbuliwa na mzio, daktari alisema, mzio. Kama hiyo ni kweli, punga mkono wako namna *hii*, ili waweze . . . Unaamini? Kweli alikuwa nao, hana sasa, umemwacha, mnaona. Yeye hajui hilo bado. Hebu na ajue hilo, unaona. Yeye ni mtu mzuri. (Usifasiri hilo.)

251 Huyu hapa akija tena, huyu hapa anarudi mbele yangu. Nena sasa, unaona wakati mimi . . . Una mtu mwingine moyoni mwako. Unamwombea mtu fulani. Hivi unaamini ya kwamba Mungu angali anajua siri ya moyo? Bi—Biblia ilisema Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, ukiyatambua mawazo ya moyo. Hiyo ni kweli.

252 Unamwombea mama yako. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Mama yako, unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia mama yako ana shida gani? Ana shida ya kina mama, inayoitwa shida ya kike. Kama hiyo ni kweli, punga mkono wako. Unataka nikwambie mahali alipo? Hayupo hapa, yuko Tijuana. Yote yamekwisha, Yeye ameponywa. Nenda, mwamini Yeye sasa katika Jina la Bwana Yesu.

Hebu na tuseme, "Bwana asifiwe," kila mtu. Amininі, msiwe na shaka. "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu."

253 Hebu kidogo. Yuko wapi msichana huyo mdogo? Njoo hapa. Mtu huyo aliyeinua mkono wake juu, aliyeketi hapa nyuma, papa hapa mwishoni mwa benchi hili, papa hapa mwishoni, yeye hazungumzi Kiingereza, bali anaomba, anamwombea mpendwa, dada yake. (Kaa hapo. Hebu aje. Sasa mwambie asimame papo hapo.)

254 Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Kama nitakufunulia kile unachoombea, utamwamini Bwana Yesu? Je, una kadi ya maombi? Huna kadi ya maombi? Huhitaji moja. (Mwambie yeye haihitaji, la, haina haja.) Niangalie, angalia

hapa. Una imani nzuri. Huhitaji kadi ya maombi. Uligusa vazi Lake.

255 Ulikuwa ukimwombea mtu fulani mgonjwa sana, dada yako. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yake ni nini? Ana TB. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, punga mkono wako. Chini huko Nogales. Punga mkono wako, ili. . .Mtumie neno ya kwamba Yesu Kristo anamponya, kama atakubali uponyaji wake. Amina.

Unaamini kwa moyo wako wote sasa? Mungu akubariki. Ninampa changamoto yeyote. . .Aligusa nini? Aligusa nini?

256 Yule mtu aliyekuwa akijaribu kumsaidia mtu yule mwingine pale, bwana, ulimpa Mungu fadhila, ulisaidia. Ulikuwa ukijaribu. . .Naam, ukijaribu kuwaambia nanii wako. . .Si lazima uje, simama papo hapo, unazungumza Kiingereza. Una kadi ya maombi? Huna. Vema, kama utaamini kwa moyo wako wote, hiyo ngiri itakuacha, unaweza kwenda nyumbani, uwe mzima.

257 "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Vema, hivi hamjui Yeye yupo hapa? Hivi hamjui huyo ni Yeye? Mwaminini Mungu. "Kama unaweza kuamini, yote yanawezekana."

258 Hatufahamiani. Sikujui, nawe hunijui, lakini Mungu anatujua sote wawili. Sasa amini, usiwe na shaka, amini. Kama utaamini, mambo yote yanawezekana. Sijawahi kukuona maishani mwangu, bali Mungu anakujua, na kama anaweza kunifunulia jambo fulani ambalo umefanya, ama jambo fulani unalotaka, ama kitu fulani unachotamani, ama kadhalika, unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama, ninamaanisha mtumishi Wake? Neno *nabii* huwakwaza watu mara nyingi, mnaona, kwa hiyo sisemi chochote.

259 Je, Biblia. . .? Unasoma Biblia sana? Biblia inasema, ya kwamba Neno la Mungu ni kali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena hukata hata kugawanya, hata kwenye mafuta yaliyomo ndani ya mfupa, na Mtambuzi wa mawazo ya moyo. Hiyo ni kweli? Vema, Neno ni nini? "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu." Kwa hiyo basi ni Yesu Kristo ndani yetu, akiyatambua mawazo ya moyo, Neno lililofanyika mwili miongoni mwetu usiku wa leo. Mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema, na Mungu wa Mbinguni akifasiri mawazo yenyewe ya moyo wako, na kuwaponya wagonjwa.

260 Wewe ni mgonjwa sana. Una tumbo lenye vidonda. Hiyo ni kweli. Inua mkono wako. Hiyo ni kweli. Kuna wengi sana wao huko nje kwenye kusanyiko, inatawanyika tu kila mahali. Inasababishwa na hali ya wasiwasi. Hapa, hebu niwaonyeshe jambo fulani. Hebu tuone jinsi wewe. . .

261 Kila mtu huko nje anayeugua ugonjwa wa wasiwasi, inueni mikono yenu, iweni waaminifu. Nitawaitaje, mnaona? Haya basi. Mnaona, inakuja tu kama wimbi kubwa sasa, kila mahali. Loo, Bwana wetu Yesu!

262 Una tumbo lenye vidonda, na pia una ugonjwa wa moyo. Daktari alikupa dawa unywe, lakini huwezi kuinywa. Inatoa ugiligili ndani yako, wala huwezi kunywa dawa yako. Hutoki hapa, umetoka nchi nyingine baridi, unatoka jimbo la Ohio, mji unaoitwa Youngstown. Jina lako ni Bibi Mink. Unaye mume aliye na kisukari. Nenda ukiamini, naye Bwana Yesu atakuponya.

263 Unaamini, moyo wako wote? Hilo linapaswa kuwa la kushawishi. Usipoamini sasa, kamwe hutaamini. Unaona? Kama ukiamini kwa moyo wako wote sasa hivi, unaweza kukubali . . .

264 Sasa, usi—usifanye hivyo. Unaona? Mnazunguka-zunguka. Hiyo inararua tu . . . Itanibidi tu kusimama. Mnaona? Hiyo ni . . . Vema, muda si muda mwajua mwanangu atakuwa akinipiga-piga ubavuni, na hiyo inamaanisha niondoke. Mnaona? Iweni na kicho. Tulieni tu mara moja zaidi, sivyo? Ndipo tutawaomba tu wawekeane mikono. Mnapoamka namna hiyo, mnaona, inamhuzunisha Roho Mtakatifu, nami ninapata . . . anaondoka kwangu, wala si—siwezi kumzuia. Mnaona? Maana Yeye huhuzunika, Naye huniacha. Mnaona?

265 Hamna budi, kama mnaniamini, mtafanya yale ninayowaambia mfanye. Hamnitii mimi, mnamtii Yeye kupitia sauti yangu, ninapozungumza nanyi. Mnapoamka na kusogea namna hiyo, mnakatiza tu, vibaya sana. Mnaona? Ni vigumu kushikilia Uwepo wa Roho Mtakatifu. Msipoamini, basi mnaamka tu na kutembea huku na huku na kusogea, ina—inaumiza. Mnaona?

266 Huyo mama hapo, unayesumbuliwa na mikono na mabega yako, sijawahi kukuona maishani mwangu, mama, aliyeketi papa hapa na leso usoni mwake. Unaona? Mwamini tu Mungu. Una ja—jamaa, ama mpendwa anayesumbuliwa na miguu yao, ni shemeji yako. Amini na usiwe na shaka.

267 Hatufahamiani, bwana. Hii . . . Mungu anatujua sote wawili. Sasa, wakati ninii . . . Kadiri niwezavyo kukumbuka, wewe ndiye mwanaume wa kwanza ambaye amekuwa hapa jukwaani usiku wa leo, kadiri nijuavyo mimi, nafikiri kuna wengine zaidi kote kwenye kusanyiko, lakini wa kwanza ninayemjua. Sasa, kama Bwana Yesu atafanya mambo yale yale kama alivyofanya wakati Simoni alipomjia, na kuniambia shida yako, ama kilichokuleta hapa, unaniamini mimi kama mtumishi Wake?

268 Je, hili litawashawishi, wanaume wote, kama vile wanawake walivyofanya? Sasa, mnaona, hao watu huko nje hawana kadi za maombi. Mnaona, haijalishi, mguseni tu Yeye, semeni tu, “Bwana, acha iwe ni mimi.”

269 Huh! Huyo mama aliyeketi papo hapo, alisema jambo lile lile wakati uo huo, anasumbuliwa na ugonjwa wa ini, ulikuacha. Gauni hilo lenye milia, mwanamke mnene, umekuwa ukisumbuliwa na ugonjwa wa ini, sivyo? Ulisema, "Bwana, acha iwe ni mimi." Inua mkono wako sasa kama ndivyo ilivyo. Vema, imekwisha.

270 Aligusa nini? Mnaona jinsi alivyo mbali nami? Futi thelathini ama arobaini, bali aliamini. Niliona ini hilo legevu likishuka chini namna *hiyo*, ni sawa. Amini, utapona sasa.

271 Samahani, bwana, inanibidi tu kufuata jinsi Roho aongozavyo, mnaona, nami. . . Unasumbuliwa na shida ya tumbo, hiyo ni kweli, bawasiri. Una baadhi ya mambo unayojaribu kuweka chini na kuyaacha, tabia, hiyo ndiyo inayosababisha shida yako ya tumbo. Umeponywa hapo awali, kansa. Acha kuvuta sigara, kuwa mvulana mzuri, mwamini Bwana Yesu. Aisee, ninamwona mwanamke amesimama karibu nawe, ni mke wako, yuko tayari kufanyiwa upasuaji, ugonjwa wa kike. Wewe hutoki kwenye mji huu, unatoka Phoenix. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Ungeamini kwa moyo wako wote? Bw. Sparrow, rudi Phoenix, ukaponywe katika Jina la Yesu Kristo.

Mnaamini kwa moyo wenu wote kila mtu? Vema, hilo—hilo linatosha basi, hilo tu ndilo mnalohitaji.

Kama utamwamini Mungu, hutakuwa na yabisi kavu tena. Nenda, mwamini kwa moyo wako wote, na upate afya.

Kama unamwamini Mungu, ugonjwa wa moyo utakuacha. Nenda, amini kwa moyo wako wote, na uamini hilo.

Mnaamini huko nje, kila mmoja wenu? Iweni tu na imani, hivyo tu ndivyo inavyowapasa kufanya.

272 Sasa, mama, ulipofika kule juu muda mfupi uliopita, ulikuwa umechanganyikiwa kabisa, ugonjwa huo wa mgongo utakuacha, kama utaamini. Endelea, uponywe, na uamini. Amini tu, na kusema, "Mungu, ninaamini kwa moyo wangu wote."

273 Utakufa kama kansa hiyo haitaponywa, lakini kama Mungu angeweza kumponya mmoja kansa, ataiponya kwa mwingine. Unaamini? Vema, basi nenda, na uamini kwa moyo wako wote, na Mungu hakika atafanya hivyo. Amina.

274 U hali gani, mpenzi? Unaamini? Njoo hapa. Nafikiri wewe ni mmoja wa wasichana wadogo warembo sana niliowahi kuona, karibu kama wangu, nina msichana mdogo nyumbani, Sarah. Sasa, angalieni, Yesu anawapenda wasichana wote wadogo. Unaamini hilo? Sasa, kama Yesu angekuwa hapa, Yeye angesema . . . Yeye alisema, "Waacheni watoto wadogo waje Kwangu, msiwazuie." Naye angeweka mikono Yake juu yako, nawe ungepona. Unaamini hilo, sivyo? Hakika, ungefanya hivyo.

275 Sasa, Yesu yuko kwenye mkono wa kuume wa Mungu Mbinguni, bali Yeye huwatuma watumishi Wake kurudi kufanya jambo hilo. Kwa hiyo sasa, mtumishi, Yeye alisema, "Kama mtumishi huyu akisema ya kwamba nimemtuma, naye hatendi kazi Zangu, basi amekosea. Lakini kama akizifanya hizo kazi, hiyo inamaanisha nilimtuma."

276 Sasa, Yesu alikuja kukuponya. Sasa, kama Yeye ataniambia shida yako ni nini, utamwamini, kisha uende nyumbani, uwe mzima? Basi hutakohoa tena, wala haikulazimu kunywa Asthmador tena, maskini hiyo pumu itakuacha, katika Jina la Bwana Yesu. Amina. Kuwa na imani.

277 Njoo, mama. Unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini kama Mungu ataniambia shida yako, utalikubali kwa ajili ya uponyaji wako? Basi shida hiyo ya kina mama, shida ya kike, umekuwa nayo, nenda, amini, nayo itakuacha. Amina.

278 Njoo, mama. Imekuwa muda mrefu tangu ulipoweza kula, na kula vizuri. Tumbo lako limekusumbua. Nenda ukale sasa, Yesu Kristo anakuponya. Kuwa na imani . . .? . . . Mungu akubariki.

Uko hapa nje kwa ajili ya hiyo pumu, ukifikiri itakuacha. Lakini Mungu ni Mponyaji, Yeye yuko kila mahali, kwa hiyo nenda tu, na uamini, Kasisi.

Unaamini kwa moyo wako wote? Punga mkono. "Kama unaweza kuamini, yote yanawezekana." Mwaminini Mungu.

279 Jambo fulani lilitukia, siwezi—siwezi kulipata. Unayeketi hapo umevaa koti hilo jeupe, hilo hapo. Ningeweza kuona koti hilo, bali nisingeweza kujua lilikuwa wapi. Vema, ugonjwa huo wa kibofu nyongo utakuacha sasa. Vema. Unaweza kwenda nyumbani, ukaponywe.

Moja kwa moja hapa chini kwa ajili ya kifafa. Unaamini Mungu ataponya kifafa?

280 Huyo hapo mwingine ameketi huko nyuma, jamaa huyo mdogo aliyevaa suti ya bluu, ameinua mkono wake. Unaamini Mungu ataponya kifafa, ndugu? Simama na ukubali uponyaji wako. Aminini ya kwamba Yesu . . . Naam. Uligusa nini, yadi thelathini kutoka kwangu?

281 Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, yupo hapa. Unaamini hilo? Ningewezaje kufanya hivyo? Mimi ni ndugu yenu. Ni wangapi wenu walio waaminio? Inueni mikono yenu. Vema. Je, Yesu anasema hivi, agizo la mwisho kwa kanisa: "Enendeni ulimwenguni kote, na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio?" Je, Yeye alisema jambo hilo? Je, wewe ni mwaminio? Yeye alisema nini? "Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Hiyo ni kweli?

282 Basi wekeaneni mikono sasa hivi, nao wataninii . . . itaninii . . . mtaenda sawa, na kila mmoja wenu aponywe. Wekeaneni mikono, popote mlipo, wekeaneni mikono. Huko

juu kwenye roshani, fanyeni vivyo hivyo, wekeaneni mikono. Haya basi. Sasa, usijiombee mwenyewe, huyo mtu mwingine anakuombea, wewe—wewe mwombee awe mwanaume au mwanamke. Sasa, Biblia ilisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Sasa omba jinsi unavyoomba kanisani mwako, useme, "Mungu, mponye mtu huyu, wape afya."

283 Baba wa Mbinguni, ninakuletea Wewe, katika nguvu za kufufuka kwa Mwanao Yesu Kristo, kusanyiko hili. Ninamlaani ibilisi, ninalaani kutokuamini, ninamtoa yule mwovu.

284 Toka, Shetani, umeshindwa vita. Umefichuliwa hapa, usiku wa leo, mbele ya watu hawa, kuonyesha ya kwamba huwezi kusimama, ufalme wako umekwisha, unaporomoka. Yesu Kristo yuaja, na Uwepo Wake upo hapa usiku wa leo kudhihirisha nguvu Zake. Ninakuamuru, katika Jina la Yesu, toka ndani ya watu hawa, na uwaache waende.

285 Kila mwanamume na mwanamke humu jengoni ambaye sasa unaweza kuamini kwamba umeponywa, simama kwa miguu yako na ukubali uponyaji wako, ninatangaza umeponywa katika Jina la Yesu Kristo. Simameni na mumpe sifa.

61-0205E Yesu Kristo Yeye
Yule Jana, Leo, Na Hata Milele
Central Assembly Of God
Tucson, Arizona Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org